SportPesa
TZS. 985,669,400
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Wasiojulikana** wakata viungo vya maiti, makaburi yavunjwa

UKURASA 3

Nipashe

Jumanne Machi 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580871

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## TUCHEL AKATAA KUMLAUMU KEPA

UKURASA 22



# Nafuu ya mafuta yaja kwa miezi 3

• **Serikali** yakubali kupata hasara ya bilioni 30/- kila mwezi... *Endelea ukurasa 2*




## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**NEEMA YAWAANGUKIA WAKULIMA WA PAMBA**

BODI ya Pamba Tanzania (TCB), imeanza mpango wa kusambaza chupa milioni mbili za viuatilifu za kuua wadudu wanaoshambulia zao la...

UKURASA WA 5

**MAJALIWA AAHIDI USHIRIKIANO AU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Tanzania itaendelea kuunga mkono na kuimarisha ushirikiano uliopo na Umoja wa Afrika...

## TPA yapata Tril. 1/- za kuboresha ufanisi wa bandari

UKURASA 3

## Raia Ukraine waomba hifadhi kubaki Zanzibar

UKURASA 2

MICHEZO 'SABABU KIPIGO SIMBA MOROCCO HII' UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na Makamu wa Rais wa Nigeria, Prof. Yemi Osinbajo (kushoto), baada ya mazungumzo yao yaliofanyika jijini Arusha, jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Unafuu wa mafuta waja, bei kushuka

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeondoa tozo ya Sh. 100 kwa kila lita ya mafuta iliyopaswa kulipwa na watumiaji nchini kwa miezi mitatu kuanzia Machi hadi Mei, mwaka huu.

Mafuta hayo ni dizeli, petroli na mafuta ya taa, kutokana na mabadiliko hayo mapato ya serikali yatapungua kwa Sh. bilioni 30 kwa mwezi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Wizara ya Nishati, serikali itaendelea kutathmini mwenendo wa bei za mafuta katika soko la dunia.

Taarifa hiyo ilisema kuwa Waziri wa Nishati, January Makamba, aliidhinisha na kusaini marekebisho ya kanuni ili kutimiza uamuzi huo.

Aidha, ilisema: "Serikali imeona ni muhimu kuendelea kuwalinda wananchi wake dhidi ya athari za mabadiliko ya bei za mafuta ulimwenguni. Hii inatokana na ukweli kwamba endapo uamuzi huu usingechukuliwa na serikali, bei za mafuta nchini kuanzia mwezi Machi na kuendelea zingekuwa za juu sana kutokana na sababu zilizoelezwa hapo juu."

"Kutokana na kuendelea kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia kunakosababishwa na mambo mbalimbali, ikiwamo vita kati ya Urusi na Ukraine, mwenendo wa bei za mafuta nchini umeathirika kwa bei hizo kuendelea kupanda," ilisema.

Ilieleza kuwa uamuzi huo unaenda sambamba na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa baada ya kikao na wizara na taasisi mbalimbali zinazohusika na suala hilo zilizokutana Oktoba 5, mwaka jana, kujadiliana namna bora ya kupunguza bei za mafuta hapa nchini.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa kikao hicho kilikuwa kwa ajili ya kupunguza tozo mbalimbali zenye thamani ya Sh. bilioni 102 kwa watumiaji wa mafuta nchini.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, bei mpya za mafuta zitakazotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kuanza kutumika kesho zitazingatia marekebisho ya kanuni yaliyofanywa na Waziri wa Nishati.

**WADAU WAZUNGUMZA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti watumiaji wa mafuta, walipongeza serikali kwa uamuzi huo kwa kuwa unakwenda kurahisisha maisha hasa mafuta kwenye vyombo vya usafiri.

Selina Samweli, mkazi wa Dar es Salaam, alisema kuondolewa kwa kiasi hicho hasa wakati huu kuelekea Kwaresma na mfungo wa Ramadhani, kutasaidia bei ya bidhaa mbalimbali isipande.

"Bado tunaiomba serikali kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake mbalimbali kuhusu bei ya bidhaa, bado bidhaa nyingi ziko juu na sababu inayotolewa ni kupaa kwa mafuta, sasa yanashuka tunatarajia kuona vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine zinashuka,"alisema.

Naye Mariam Hussein alisema kuondolewa kwa kiasi hicho kutaleta ahueni kubwa, huku akiomba serikali kufuatilia utekelezaji kwa karibu zaidi hasa wa bei ya bidhaa na nauli za ndani pamoja na mikoani.

"Kama mafuta yameshuka basi hata nauli zishuke kwa miezi mitatu, itatusaidia, ikiwa hali itakuwa hivyo, kwa ujumla maisha yamekuwa magumu kwa kuwa kila bidhaa imepanda bei kwa sasa, huku nauli zikiwa zile zile," alisema.

## Raia wa Ukraine waomba hifadhi kubaki Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa raia wa Ukraine 900 wapo Zanzibar na kutokana na machafuko yalioko nchini mwao wameomba kuendelea kuhifadhiwa Zanzibar ombi ambalo amelikubali.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu mjini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari, katika utaratibu aliojiwekea kila mwisho wa mwezi.

Alisema raia hao Ukraine walioko Zanzibar wameiomba serikali yake kuwapatia hifadhi kwa sababu baadhi yao wamekuja nchini kwa ajili ya utalii na wamefikia katika hoteli za kitalii na fedha zimewaishia, hawana gharama ya kulipa mahitaji ya makazi katika hoteli hizo walizofikia na nchini kwao hakuendeki kutokana na vita.

Dk. Mwinyi alisema kuwa serikali yake baada ya kupokea maombi ya msaada huo kutoka kwa raia hao tayari imeshafanya jitihada za kuongea na wamiliki wa hoteli za kitalii walizofikia ili kuwasaidia kubaki bila ya kulipa gharama.

"Tunapokea watalii wengi kutoka Ukraine na kuna watalii 900 hivi sasa wapo Zanzibar na hawawezi kurudi kwao wameiomba serikali kuwasaidia hawawezi kuendelea kukaa katika hoteli kwa sababu hawana fedha...tumeanza mazungumzo ya wamiliki wa hoteli na Serikali ya Zanzibar kuwasaidia mpaka serikali yao itakapopata uwezo wa kuleta msaada," alisema.

Alisema kuna makubaliano ambayo yameanza kuonekana wenye hoteli kuwapa msaada bila ya kuwalipisha gharama, lakini pia serikali kuwaangalia wenye hoteli kwa upande wa kodi.

Alisema serikali imeona umuhimu wa kutoa msaada kwa raia hao ambao walioko kwao wanaondoka kwa kuwa huwezi kuwaambia warudi kwao ni lazima kutafuta njia za kuwasaidia.

Akizungumza kuhusu mfumuko wa bei za vyakula hasa kuelekea mwezi wa Ramadhani, alisema serikali imepitia kodi zinazotozwa katika chakula na imefanya uamuzi wa kupunguza katika bidhaa ya sukari.

Alisema sukari ilikuwa inatozwa asilimia 15 ya kodi la Ongezeko la Thamani (VAT) na asilimia 25 ya uagiziaji bidhaa na kupunguza na kwa sasa itatozwa asilimia 12.5 ili kushusha gharama za bidhaa hiyo katika soko.

"Wito wangu kwa wafanyabiashara wote wanaouza bidhaa hizi za chakula waone nia njema ya serikali ya kupunguza kodi kwa kiwango kikubwa ili bidhaa hizo zipatikane kwa nafuu Unguja na Pemba," alisema.

Alisema kuwa bei ya sukari imewekewa bei elekezi na kwa Pemba isizidi Sh. 2,000 kwa kilo moja ya sukari na kwa Unguja isizidi Sh. 1,900 tofauti hiyo inatokana na gharama ya usafiri kutoka Unguja kwenda Pemba.

Dk. Mwinyi aliitaka Tume ya Ushindani kutimiza wajibu wao kupita kila duka kuhakikisha bei elekezi inasimamia na wasipofanya kazi hiyo, lazima serikali itachukua hatua dhidi yao kwa sababu imepewa jukumu kisheria la kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kuzuia mfumuko wa bei usiokuwa na sababu.

Aidha, akizungumzia kuhusu boti zilizonunuliwa na serikali yake kwa ajili ya usafiri kwa wananchi wa visiwa vidogo vilivyomo ndani ya Zanzibar, alikiri kuwa amepokea taarifa ya kuwa boti hizo hasa kisiwani Pemba hazitumiki vizuri kwa sababu walikuwa wanasafirisha watu na kulalamika kuwaondolea biashara zao.

"Pia kuna utata juu ya nani atalipa mafuta ya boti hizi mpya za serikali wakati zilitakiwa kusafirisha kwa gharama ndogo ili kupatikana mafuta na kuzifanya boti hizo kuwa endelevu, lakini tutaendelea kusimamia jambo hili ili kufanya kazi iliyokusudiwa kwa gharama nafuu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema serikali ilitangaza kuziuza meli za Shirika la Meli Zanzibar ambazo hazifanyi kazi, lakini bado hazijapata mteja kwa sababu ya Maendeleo na Mkombozi namba moja hazifai kuuzwa kwa ajili ya kuendelea na safari labda ziuzwe kama vyuma chakavu.

Kuhusu meli ya Mapinduzi namba mbili ambayo ilinunuliwa mwaka 2015, alisema haiuziki kwa sababu imenunuliwa kwa gharama kubwa na serikali inatafuta njia mbadala ili kutafuta watu kuitengeneza na kuikodisha au kuibadilisha na kuifanya hoteli.

## Wenye ualbino walia kukosa wachumba

**Na Richard Makore,** MWANZA

BAADHI ya wanawake wenye ualbino mkoani Mwanza, wameiomba serikali kuelimisha wanaume ili wabadilike wawaoe kwa kuwa wanapata shida kupata wachumba.

Kadhalika, wameitaka jamii kuachana na imani potofu kwamba mwanaume akifanya mapenzi na mwanamke mwenye ualbino atapona ugonjwa wa Ukimwi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza jana katika kikao cha kamati ya amani ya viongozi wa dini, mmoja wa wanachama wa Chama cha wenye Ualbino mkoani Mwanza, Monica Yusuph, alisema kundi hilo linapata shida kupata wanaume wa kuwaoa.

Alisema kwa muda mrefu jamii hususani wanaume wamekuwa wakikwepa kuwaoa wanawake wenye ualbino bila sababu za msingi.

"Sisi wanawake wenye ualbino hatupati wanaume wa kututongoza ili hatimaye kutuoa, hivyo tunaiomba serikali kuweka nguvu katika kutoa elimu kwa jamii kwamba watu hao hawana tofauti na wanawake wengine wasiokuwa na ulemavu," alisema.

Kuhusu imani ya kufanya mapenzi na mtu mwenye ualbino mwanaume atapona Ukimwi, Monica alisema hakuna kitu kama hicho bali hatua hiyo itazidi kueneza ugonjwa huo katika jamii.

Akizungumzia tatizo hilo kwa watu wenye ulbino, Katibu wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wa Ngozi mkoani Mwanza, Anjelina Chuma, alikiri kukumbana na unyanyapaa, na kwamba mchumba, lakini jamii ikawa inamcheka mwanaume huyo kwa nini ameamua kuwa na mahusiano na mwenye ualbino.

Aliongeza kuwa kutokana na kuongeza kwa dharau, mume wake aliamua kumuacha licha ya kuwa alizaa naye mtoto.

Aidha, aliomba jamii iendelee kupatiwa elimu kwamba hakuna tofauti kati ya mwanamke albino na yule asiyekuwa na hali hiyo.

Mjumbe wa kamati ya amani ya viongozi wa dini mkoani Mwanza, Askofu Charles Sekelwa, alisema wataendelea kuhubiri upendo kwa jamii nzima.

Aidha, alisema licha ya mauaji ya watu wenye ualbino kupungua nchini, lakini wataendelea kukemea vitendo hivyo kuhakikisha watu hao wanaishi kwa amani kama watu wengine.

Alisema umefika wakati jamii kuachana na unyanyapaa wa aina yoyote na badala yake wawape fursa za uongozi wenye ualbino katika nyumba za ibada.

Aliiomba serikali kutoa mrejesho wa wenye ualbino waliokimbia makazi yao kwa kuhofia usalama wao, na kwamba hatua hiyo itasaidia kujua namna ya kuwapatia huduma muhimu za kijamii, ikiwamo elimu na afya.

**Kuhusu imani ya kufanya mapenzi na mtu mwenye ualbino mwanaume atapona Ukimwi, Monica alisema hakuna kitu kama hicho bali hatua hiyo itazidi kueneza ugonjwa huo katika jamii.**

# TPA yapata shilingi trilioni 1.1 kuboresha ufanisi wa bandari

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kimataifa ya Uchukuzi na 'Logistic' ya DPW ya Umoja wa Falme za Kiarabu itatumia Dola za Kimarekani milioni 500 (sawa Sh. 1,161,086,870,197) katika miradi mbalimbali iliyolenga kuboresha ufanisi katika bandari zinazomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Taarifa iliyotolea na TPA jana, ilisema makubaliano ya kupatikana kwa fedha hizo yalitiwa saini katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dubai (Dubai Export 2020) kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania TPA, Eric Hamissi na Mtendaji Mkuu wa DPW, Sultan Ahmed Bin Sulayem.

Ilisema makubaliano ya ushirikiano (MoU) yaliyofikiwa ni sehemu ya matukio muhimu wakati wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, nchini Dubai aliyehudhuria Siku ya Tanzania katika maonyesho hayo juzi.

Fedha zilizopatikana zitatumika kuendeleza Bandari za Tanzania kwa kuimarisha mifumo ya TEHAMA, mafunzo kwa watumishi na uendelezaji wa miundombinu ya kibandari katika Bandari za Mwambao wa Bahari na Maziwa.

Fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya kuiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuongeza ushindani wake katika viwango vya kimataifa vya ubora na ufanisi wa huduma.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Airtel Afrika, Olusegun Ogunsanya (watatu kulia) pamoja na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Airtel Afrika Mashariki, Ian Ferrao (wapili kulia), nchini Dubai juzi. **PICHA: IKULU**

# Viungo vya maiti vyakatwa, makaburi yavunjwa Magu

**Na Richard Makore,** MAGU

WATU wasiojulikana wamevamia makaburi ya serikali wilayani Magu, mkoani Mwanza na kuvunja majeneza huku wakikata baadhi ya viungo vya maiti na kuondoka navyo.

Kadhalika, katika uvamizi huo watu hao wamedaiwa kuvunja makaburi yaliyojengwa kwa kutumia zege kisha kuchukua nondo na misalaba ya chuma kwa lengo la kwenda kuviuza kama vyuma chakavu.

Hatua hiyo imeiweka serikali wilayani humo katika tahadhari na kuagiza ufanyike msako ili kuwabaini wanaofanya vitendo hivyo vya kiovu.

Tayari serikali imelaani na kukemea vitendo ambavyo imeviita vya kikatili na visivyokuwa vya kawaida katika tamaduni za kitanzania.

Kutokana na vitendo hivyo, watu kadhaa wamekamatwa na kufikishwa mahakamani huku msako ukiendelea ili kuwabaini wengine wanaodaiwa kufanya uhalifu huo.

Ofisa Habari wa Wilaya ya Magu, Pascaly Mashamba, ameiambia Nipashe kwamba watu hao walikamatwa hivi karibuni kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo hivyo vya kikatili vya kubomoa makaburi.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, amekiri kuwapo kwa vitendo hivyo, baada ya kutembelea eneo hilo akiwa ameambatana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini waliofanya tukio hilo la kinyama ni watu wanaotafuta nondo na misalaba kwa lengo la kwenda kuviuza kama vyuma chakavu.

Wakati mkuu huyo wa wilaya akitoa onyo hilo, kumebainika pia watu hao walivunja majeneza na kukata baadhi ya viungo vya maiti na kuondoka navyo.

Kwa takribani wiki moja sasa, mkuu huyo wa wilaya, aliagiza ufanyike msako ili kuwabaini watu wanaofanya vitendo hivyo vya kikatili.

Akizungumza na Nipashe, Kali alisema msako wa kuwasaka watu hao umeanza na ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya kazi hiyo usiku na mchana ili kuendelea kuwabaini watuhumiwa hao.

Alisema alipokea taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu kuwapo uvunjaji wa makaburi hayo na kwamba alifika huko haraka na kukuta makaburi yaliyovunjwa yakiwa wazi.

Alisema watu hao wanavunja misalaba iliyotengenezwa kwa nondo pamoja na kubomoa zege la juu kisha kuchomoa nondo zote.

Kali akiwa katika ziara ya kuhamisha matumizi ya anwani ya makazi katika eneo hilo, alisema, ni lazima watu hao wakamatwe ili iwe fundisho kwa wengine.

Kutokana na hali hiyo, kwa sasa umeimarishwa ulinzi wa mgambo ambao wameagizwa kulinda makaburi hayo wakati ndugu wa marehemu waliozikwa hapo wakifanya utaratibu wa kuyajengea upya.

# Neema yawaangukia wakulima wa pamba

**Na Happy Severine,** BARIADI

BODI ya Pamba Tanzania (TCB), imeanza mpango wa kusambaza chupa milioni mbili za viuatilifu za kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba katika Mkoa wa Simiyu.

Idadi hiyo ya chupa ndiyo mahitaji halisi ya wakulima mkoani humo na katika awamu ya kwanza zimewasili chupa 600,000.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi magari yaliyobeba dawa hizo kwa uongozi wa mkoa huo, mwakilishi wa TCP, Said Juma alisema zinatosha kwa wakulima wote mkoa mzima.

Alisema kuwa kwa awamu ya kwanza, wamepokea magari yanye chupa 600,000 huku kiasi kingine cha sumu kilichobaki kikitegemewa kuwasili ndani ya wiki hii.

Aliongeza kwamba viuatilifu hivyo ambavyo vimeanza kupokelewa vitaanza kupelekwa kwa wakulima ili kupulizia kutokana na wadudu kuanza kushambulia zao la pamba.

"Sasa hivi ndicho kipindi cha kupulizia viuatilifu kwani wadudu wanaanza kushambulia pamba, baada ya zoezi hili la kuvihifadhi vitatakiwa kuanza kupelekwa kwa wakulima moja kwa moja," alisema Juma.

Aidha, Juma aliwatoa wasiwasi wakulima wa zao hilo kuwa bodi imejipanga kikamilifu kuhakikisha kila mkulima anapata dawa za kutosha.

"Wakulima wasiwe na wasiwasi, dawa zipo za kutosha na kila mkulima atapata dawa kulingana na shamba lake, tunawaomba mara watakapopata dawa waanze kupulizia mara moja," alisema Juma.

Alizitaka kamati mbalimbali kuanzia ngazi ya kitongoji hadi wilaya kudhibiti wizi wa dawa hizo katika mkoa huo.

"Katika usambazaji wa awali kumetokea sumu hizi kuibiwa na kufanyiwa biashara, tunatoa rai na tahadhari kwa yeyote atakayehusika hatua kali za kisheria dhidi yake zitachukuliwa," alisema

"Kule wilayani hadi vitongoji, kuna kamati ambazo zinahusisha wakulima wenyewe na viongozi wa serikali, ambazo zinadhibiti jambo hilo, ni wakati sasa wa kamati hizi kuanza kufanya kazi ili kila mkulima apate dawa kulingana na shamba lake," alisema Juma.

Akipokea magari yenye viuatilifu hivyo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, David Kafulila, Katibu Tawala Msaidizi (miundombinu), Mashaka Luhamba, alisema wamepata dawa hizo kwa wakati mwafaka.

Luhamba alisema kuwa kama mkoa walifanya juhudi za kuhamasisha wakulima walime pamba na wengi waliitikia, hivyo kuletwa kwa dawa hizo kuwawezesha kufikia malengo yao ya kuzalisha tani 150,000.

"Baada ya kupokea sumu hizi, bila ya kuchelewa leo (jana), zinaanza kupelekwa kwa wakulima, tayari tumetoa maelekezo kwa wakuu wa wilaya kusimamia zoezi la ugawaji na kuhakikisha kila mkulima anapata dawa," alisema Luhamba.



Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, Seleman Bishagazi, akichangia hoja katika semina ya jinsia na maendeleo (GDSS) iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Mabibo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Bashungwa awaagiza ma-RC kituo kimoja huduma kwa wateja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amewaagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha wanaanzisha kituo cha pamoja cha huduma kwa wateja.

Bashungwa alitoa maelekezo hayo jana alipofanya ziara ya siku moja mkoani Pwani ambapo alitembelea ofisi ya mkuu wa mkoa pamoja na kukagua mradi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Msingi Tumbi na Sekondari ya Kibaha zilizo chini ya Shirika la Elimu Kibaha.

Alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kwa kutekeleza agizo ambalo alilitoa hivi karibuni la kila mkoa kuanzisha kituo cha pamoja cha huduma kwa wateja.

"Nawaagiza wakuu wa mikoa kuiga Mkoa wa Pwani kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja hii inarahisisha wananchi kupata huduma kwa taasisi zaidi ya moja sehemu moja," alisema.

Baada ya kukagua miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa alipongeza utekelezaji wake ambao umezingatia thamani ya fedha zilizotolewa.

Akizungumzia suala la utatuzi wa vikwazo katika sekta ya elimu, alisema katika mwaka wa fedha ujao bajeti itatoa kipaumbele kwenye ujenzi wa nyumba za walimu na kushughulikia kero zao na kuboresha mazingira ya kazi.

Akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibaha aliwataka kutumia vizuri muda wao kusoma kwa bidii ili waje kuwa wasomi wazuri wa baadaye.

Waziri Bashungwa pia alitoa maelekezo kwa Shirika la Elimu Kibaha kujipambanua kwa kubuni vyanzo vya mapato na mbinu za kutumia vizuri eneo la shirika hilo katika shughuli za maendeleo.

Awali akitoa taarifa kwa Waziri, Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Robert Shilingi, alisema wanakabiliwa na kikwazo cha ufinyu wa fedha pamoja na uchakavu miundombinu.

Shirika la Elimu Kibaha linamiliki Shule ya Sekondari Kibaha, sekondari ya wasichana Kibaha, sekondari ya Tumbi, Shule ya Msingi Tumbi, Chuo cha Sayansi, Hospitali ya Tumbi na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi.

# Bodi ya Korosho yaonyeshwa njia kufikia malengo

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ameitaka Bodi ya Korosho nchini (CBT) na wadau wa ubanguaji wa zao hilo kila mmoja kudai matokeo ya malengo waliyojiwekea kabla ya kufikiria kuwa na malengo mapya.

Amesema bila ya kujua matokeo yaliyofikiwa katika malengo ya nyuma juu ya mafanikio na kutokufanikiwa katika viwango walivyojiwekea kwenye ubanguaji wa korosho, itakuwa ni vigumu kufikia malengo mapya.

Brigedia Jenerali Gaguti, alitoa kauli hiyo jana mkoani hapo, alipofungua kikao cha wadau wa ubanguaji korosho kilichokuwa na lengo la kujadili mbinu mbalimbali ya kuongeza ubanguaji wa zao hilo.

"Bodi mmefanya kikao mwaka jana na mwaka huu mmefanya tena hiyo ni dhamira ya dhati ninawapongeza na niwapongeze wadau wote wa korosho kwa tathmini yangu tumefanya vizuri kwenye tasnia hii kwa mwaka huu hatukuwa na kelele kama miaka mingine kwani kulikuwa na utulivu wa kutosha," alisema Brigedia Jenerali Gaguti.

Kadhalika, alisema ni wakati wa kutumia utulivu huu kufikia malengo mengine ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha ubanguaji na kukitaka kikao hicho kiwe ni cha kufanya uamuzi wa kupata matokeo ya malengo wanayojiwekea na wapi wamekwama.

Alisema miongoni mwa uamuzi huo ni kukubaliana kupata mrejesho wa kila jukumu lililochukuliwa na mdau wa ubanguaji na namna alivyotekeleza ikiwamo wenye viwanda kwa kile alichoeleza ni aibu nchi kuwa na viwanda vya ubanguaji 49 huku zaidi ya nusu yake zikiwa hazifanyi kazi hiyo. Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho nchini Brigedia Jenerali mstaafu Aloyce Mwanjile kwa upande wake, alieleza kuwa katika kikao kama hicho walichokaa Septemba mwaka jana, walikubaliana kuongeza ubanguaji wa korosho, kutoka asilimia 10 za sasa hadi 60, ifikapo 2025/2026.

Alisema katika msimu wa 2021 viwanda na vikundi vya ubanguaji korosho kwa ujumla wake vilibangua tani 7,200 za karanga sawa na tani 28,800 za korosho ghafi huku uwezo wa mashine ukiwa ni kubangua tani 68,972.

Msimu wa 2021/2022, lengo la uzalishaji lilikuwa ni tani 280,000 na ubanguaji ulitakiwa kufikia tani 56,000 ambayo ni asilimia 20 ya uzalishaji, kulingana na malengo ya kubangua asilimia 60 ifikapo 2025/26, lakini hadi leo pamoja na kuendelea kukusanya takwimu ubanguaji uko chini sana na haina afya kwa maendeleo ya tasnia na nchi kwa ujumla," alisema.

Pia alisema serikali kupitia bodi hiyo inafahamu changamoto mbalimbali zilizoko katika ubanguaji na inazifanyia kazi kwa kuweka njia mbadala ya kukabiliana na changamoto hizo.

Alizitaja njia hizo kuwa ni pamoja na kuwapo kwa soko la awali linalotoa fursa kwa wabanguaji wa ndani kununua korosho kwenye AMCOS bila kuwapo ushindani wa wasafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi.

Aliwataka wadau kujadili kwa kina na uwazi ikiwa ni pamoja na kubaini sababu ya viwanda vilivyoacha kubangua ilhali havina uchakavu wa mashine.

Alisema sababu hizo zikijadiliwa kwa uwazi itawezesha bodi na serikali kwa ujumla kuwa na mikakati ya kufikia malengo ya ubanguaji kwa mwaka 2022/2023 ambao ni tani 115,500 sawa na asilimia 30 ya uzalishaji wa tani 385,000.

Kaimu Mkurugenzi wa bodi hiyo nchini, Francis Alfred, alisema kusafirisha korosho ghafi kwenda nje ya nchi kunanyima fursa nyingi za ajira za wazawa kwa kuwa jukumu lao litakuwa limeishia kwenye kulima na kuuza pekee.

Korosho ni ajira na kwa sasa nchi nyingi zimeongeza uzalishaji, tukitegemea kuuza korosho ghafi kwa kiwango kikubwa tutakuwa tunahamisha ajira za wananchi wetu, kwenda kwingine, lakini tukifanya shughuli zote hapahapa tutaongeza thamani ya zao hili na tutaongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema Alfred.

# Kibano wazazi wa wanafunzi wasioripoti shule

Na Mwandishi Wetu

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewaagiza wakuu wa wilaya zote kutumia mamlaka yao kukamata wazazi na walezi wa wanafunzi, ambao hawajaripoti kidato cha kwanza mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema lengo ni kuhakikisha kila mwanafunzi aliyefaulu anaendelea na masomo bila kikwazo kwa kuwa miundombinu muhimu imeshakamilika.

Alitaja takwimu za mahudhurio kwa kila darasa na kiwango chake kwa asilimia kwenye mabano kuwa ni kidato cha kwanza (93), darasa la kwanza (97) na elimu ya awali (110).

"Nimeagiza wakuu wa wilaya zote, wazazi na walezi wa watoto ambao hawajawasili shuleni,wakamatwe ili watoe maelezo watoto wao wako wapi," alisema.

Kafulila alisema wazazi na walezi hutumia watoto kama nguvu kazi shambani na sehemu nyingine kwa ajili ya kipato na kwamba wapo ambao hushawishi watoto wao kuacha shule.

Alisema lengo la mkoa ni kuhakikisha kila mtoto anakwenda shule na kwamba ni lazima kutumia nguvu kwa kuwa elimu ni haki ya kila mtoto lakini huzuiwa kwasababu mbalimbali.

Aidha, alisema wilaya inayoongoza kwa wanafunzi wengi kutoripoti ni Itilima na kwamba iko nyuma kwa kiasi kikubwa kimaendeleo.

Alisema pia walibaini baadhi ya wazazi na walezi wanapeleka watoto kuchimba madini na kwamba huwaachisha shule, ili wakafanye kazi ambapo fedha hugawana.

Kafulila alisema mkoa huo pia ulibaini wanafunzi wanaotoka kaya maskini zinazohudumiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wanashindwa kufanya vizuri kutokana na njaa.

Alisema wameamua kujenga mabweni maalum 10 kwa wanafunzi hao kuhakikisha wanapata chakula shuleni, kwa kuwa njaa inawafanya washindwe kusoma kwa bidii na kufanya vizuri.

Alisema mabweni manne yatajengwa na halmashauri na sita yatajengwa kwa msaada wa kampuni inayojenga reli ya kisasa ya SGR.

"Siku moja nasafiri nikapita Singida akaja binti mmoja anaomba fedha ya chakula, nilivyoongea naye alinieleza anaishi na bibi wanapata fedha za TASAF ila shida kubwa ni chakula, hivyo anatumwa kutafuta chakula... niligundua hata Simiyu kuna watoto hawana uhakika wa kula mchana, wanasoma wanatakiwa wafaulu, siyo rahisi kuvumilia njaa kali," alisema.

Kwa mujibu wa Kafulila, lengo lake ni kuhakikisha anajenga picha kubwa kwamba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ijayo ya uchaguzi kuwa watoto kutoka kaya maskini wakae bweni ili wapate chakula, na kwamba wakiwa na uhakika wa kula watafanya vizuri shuleni.

Aidha, aliwaomba wadau mbalimbali wa ndani na nje ya mkoa huo kuchangia ujenzi wa mabweni hayo, kuwezesha wanafunzi kukaa shuleni na kuwa na uhakika wa chakula, kwa kuwa kaya zao haziwezi kumudu na kwamba taifa linapoteza vipaji vingi.

# Tanzania kuendelea kuimarisha ushirikiano Umoja wa Afrika misingi haki za binadamu

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Tanzania itaendelea kuunga mkono na kuimarisha ushirikiano uliopo na Umoja wa Afrika hasa katika kuzingatia misingi ya haki za binadamu na utawala bora, demokrasia na utawala wa sheria.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ufunguzi wa mkutano wa 64 wa mwaka wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Mkutano huo unafanyika jijini Arusha.

Majaliwa alisema Serikali ya Tanzania ipo tayari kuwapokea na kushirikiana nao pale watakapohitaji ushauri wa aina yoyote. Mkutano huo umefunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Shirikisho (Majimbo) ya Nigeria, Prof. Yemi Osibanjo.

Alisema Mahakama hiyo ilianzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kwa lengo la kusimamia haki za binadamu, kwa niaba ya Rais Samia alipata fursa ya kueleza dhamira ya Tanzania katika kuunga mkono jitihada za mahakama hiyo kufanya kazi.

Naye Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Shirikisho (Majimbo) ya Nigeria, Prof. Yemi Osibanjo, akizungumzia kuhusu ajenda 2063 ya Umoja wa Afrika inayolenga kulifanya Bara la Afrika kuwa bara lenye nguvu duniani katika siku zijazo amesema kuwa ipo haja ya kutambua changamoto zinazokabili Bara la Afrika ili waifikie Afrika wanayoitaka.

Kadhalika alisema ni muhimu kuangalia namna ya kutafsiri yote yaliyoainishwa kwenye agenda 2063. "Lazima tutumie fursa na taasisi zote tulizonazo ili tuweze kufikia Afrika tunayoitaka lengo ni kuhakikisha tunaona maisha ya Waafrika yanaboreshwa na uchumi unakua."

Kwa upande wake, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, Jaji Imani Aboud, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano wanaoupata ambao unawawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.




Baadhi ya wafanyabiashara wadogo wakiendesha shughuli zao chini ya bango linalowazuia kufanya biashara kando ya barabara ya Morogoro Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Makandarasi watakiwa viwango barabara ya Manyovu - Kabingo

Na Gwamaka Alipipi

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Godfrey Kasekenya, amewaagiza makandarasi wanaojenga barabara ya Manyovu - Kasulu - Kibondo - Kabingo kuhakikisha wanaijenga kwa viwango vyenye ubora ili iweze kudumu miaka mingi.

Makandarasi hao ni CHICO anayetekeleza sehemu ya njia panda ya Nduta-Kabingo (Km 62) pamoja na Sinohydro Corporation anayetekeleza sehemu ya njiapanda ya Nduta-Kibondo Mjini (Km 25.9), pamoja na Stecol Corporation anayetekeleza barabara ya Mvugwe-Nduta (km 59.35)

Kasekenya alitoa maagizo hayo mkoani Kigoma wakati akifanya ukaguzi wa maendeleo ya mradi huo.

"Tunategemea barabara hii ikikamilika kujengwa matengenezo yake yaanze baada ya miaka 20, hivyo basi TANROADS kwa niaba ya serikali hakikisheni mnawasimamia makandarasi hawa ili tupate barabara yenye viwango vya juu," alisema Kasekenya.

Pia aliwaagiza makandarasi hao kuongeza muda wa kazi na vifaa ili kukamilisha mradi huo mapema zaidi ili kufungua Mkoa wa Kigoma kwa barabara za lami.

"Serikali itaendelea kulipa fedha za mradi kwa wakati, sasa ni jukumu lenu kuongeza muda wa kazi ili kutoongeza gharama za mradi," alisema Kasekenya.

Aidha, Kasekenya alieleza umuhimu wa barabara hiyo inayounganisha mtandao wa barabara za Afrika Mashariki kutokea Nyakanazi kwenda Kigoma kupitia makao makuu ya Wilaya ya Kibondo ikiunganisha Kasulu hadi Manyovu kwa kiwango cha lami na kutoka Kasulu hadi Burundi kwa barabara ya lami. Alisema tayari makandarasi wapo eneo la kazi kutokea Kigoma kuelekea Tabora kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Uvinza - Malagarasi (Km 51.1) na Kazilambwa - Chagu (Km.36) kwa kiwango cha lami.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Suleiman Bishanga, alisema maendeleo ya ujenzi wa barabara sehemu ya njia panda ya Nduta - Kabingo imefikia asilimia 20 na unagharimu Sh. bilioni 95.5.

Alisema sehemu ya njiapanda ya Nduta - Kibondo Mjini ujenzi umefikia asilimia 42.1 na unagharimu Sh. bilioni 31.0 na sehemu ya Mvugwe - Njiapanda ya Nduta imefikia asilimia 29.1.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hujuma kwenye miradi ya mkakati zikomeshwe

**TANGU** mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) umeanza, kumekuwa kukijitokeza vitendo visivyofaa vinavyodaiwa kufanywa na baadhi ya wafanyakazi wa mradi huo, hali inayoweza kurudisha nyuma maendeleo ya mradi.

Serikali imeanzisha mradi huo ambao ni wa kimkakati kwa ajili ya kusaidia kuinua nchi kiuchumi, lakini cha kushangaza kuwapo kwa vitendo vya hujuma ikiwamo wizi wa mafuta unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu.

Mafuta hayo ni ya magari na mitambo mingine huku wanaotuhumiwa kufanya vitendo hivyo wakidai kwamba mshahara wanaolipwa ni mdogo.

Lakini sisi tunaamini sababu za kufanya vitendo hivyo si sahihi. Ni vyema kama wanaona mshahara ni mdogo, basi wangeacha kazi kuliko kujiingizwa kwenye vitendo vinavyokwamisha miradi inayojengwa kwa fedha nyingi zinazotokana na kodi za wananchi.

Kwa mtazamo wetu, serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kufanikisha mradi huo, hivyo wanapojitokeza watu wanaouhujumu, ni wazi kwamba wanakwamisha maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla wake.

Serikali inatafuta mikopo, inatumia fedha za walipa kodi kufanya shughuli za maendeleo ukiwamo mradi huo wa treni ya umeme, hivyo kwa vitendo vya wizi, tanaamini kuwa vinatishia na kurudisha nyuma juhudi za serikali kukamilisha mradi huo wa kimkakati kwa wakati.

Watuhumiwa wa wizi huo ni vyema pia wakatambua kuwa sababu wanazotumia kuhalalisha vitendo vya wizi, hazina mashiko, kwani hata kutojua sheria haiwezi kuwa sababu ya kuhalalisha makosa.

Siku za nyuma, vitendo vya kuhujumu mradi huo viliripotiwa maeneo ya Morogoro na sasa vinazidi kushamiri na maeneo ya mkoa wa Shinyanga na Simiyu hasa kwa wizi wa mafuta yakiwamo ya magari na mitambo. Vitendo hivi ni uhujumu uchumi.

Tunadhani kwamba hujuma kama hizo si za kuvumilia, na haziwezi kuhalalishwa kwa kisingizio cha aina yoyote ikiwamo mshahara mdogo, badala yake kama mtu anaona mshahara ni mdogo, aache kazi ili nafasi yake ichukuliwe na wengine kwa kuzingatia kuwa ajira kwa sasa ni vigumu kupatikana.

Miradi yote ya kimkakati ni kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote, wanapojitokeza watu wanaoihujumu kwa kisingizio kama hicho, ni wazi kwamba wanashindwa kuwa wazalendo kwa nchi yao, hivyo sheria zilizoko ikiwamo ya uhujumu uchumi zitumike kudhibiti wahusika.

Kimsingi, tushauri kila Mtanzania kujali miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini ili imnufaishe yeye pamoja na vizazi vijavyo badala ya kuwa na ubinafsi hadi kuamua kufanya hujuma na kukwamisha maendeleo ya nchi.

Sote tunashuhudia juhudi zinazofanywa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wake kwa kuanzisha miradi mbalimbali ukiwamo huo ambao umeanza kuhujumiwa, hivyo ingekuwa ni vyema kama kila Mtanzania atatambua kuwa kinachofanywa ni kwa manufaa yake na nchi.

Hatuamiani kama mtu anayejitambua, akili timamu, mwenye uchu wa maendeleo kwa nchi yake anaweza kuthubutu kufanya vitendo hivyo vya wizi wa mafuta na vifaa vingine vinavyotumika kufanikisha mradi huo.

Tunashauri watu wa aina hiyo wasifumbiwe macho, bali ikipendekeza, msako ufanyike kila eneo lote ambalo mradi huo unapita ili kubaini vitendo hivyo na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika.

Iwapo vitendo hivyo visipodhibitiwa, inawezekana mradi usikamilike kwa wakati huku watu wachache wakineema kwa wizi na kuwaacha Watanzania walio wengi wakibaki bila kujua la kufanya.

Tunaamini kuwa serikali itachukua hatua hukakilisha miradi yote ya kimkakati kama SGR, barabara, miundombinu ya reli, viwanja vya ndege na madaraja inalindwa kwa gharama yoyote dhidi ya uhujumu, kwa kuwa ndiyo msingi na kichocheo kikubwa cha kukua kwa uchumi na nchi kupata maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Reubeni Lumbagala

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mauaji, ukatili, viongozi wa dini msinyamaze

**JUMA** lililopita, niliandika makala kwenye Nipashe iliyokuwa na ujumbe "Kamati ulinzi mwanamke, mtoto ziingie kazini kustawisha jamii".

Andiko langu lilieleza tatizo la ukatili lilivyokumba jamii na katika kupambana na ongezeko la vitendo vya kikatili, moja ya hatua iliyochukuliwa na serikali ni kuunda kamati za ulinzi wa wanawake na watoto kuanzia ngazi ya kijiji, mtaa hadi taifa na zipo kamati 18,186.

Kamati hizi zimepewa jukumu la kufuatilia na kuripoti vitendo vya kikatili ili hatua madhubuti ziweze kuchukuliwa dhidi ya washirika, wanaokiuka utu, ustawi wa watu na haki za binadamu hasa wanawake na watoto.

Mdau muhimu katika mapambano na mauaji na ukatili ni viongozi wa dini, ambao wanaheshimika na wenye ushawishi kwa waumini na jamii kwa ujumla.

Mafundisho ya viongozi wa dini yanasisitiza upendo, kuwa na hofu ya Mungu, kusaidiana, kutii sheria za Mungu na za nchi na kwa ujumla, mafundisho haya yanachangia kujenga jamii yenye kupendana na kuheshimiana.

Kutokana na kukithiri mauaji na ukatili hapa nchini, viongozi wa dini wanao wajibu wa msingi wa kupaza sauti zao katika nyumba za ibada, mikutano ya hadhara, makongamano ya dini na ya serikali, kukemea kwa nguvu zote vitendo hivi vya kinyama na kikatili ambavyo ni kinyume na mafundisho ya Mungu wanayowaeleza waamini wao.

Vilevile, wanao wajibu wa kuelimisha jamii kuwa mauaji na vitendo vya kikatili ni kinyume na sheria, kanuni, taratibu za nchi hivyo kwa kutenda vitendo hivyo si tu kuwa ni kumkosea Mungu lakini pia ni kinyume na sheria za nchi na katiba yake.

Mwaka jana nilihitimu Shahada ya Uzamili ya Sanaa Katika Elimu ya Kikisto (Master of Arts in Christian Education - MACE) kutoka Chuo cha Elam Christian University (ECU) kilichoko Mbeya.

Katika utafiti nilioufanya ili kupata shahada, niliupa kichwa "Mchango wa Viongozi wa Kanisa katika Kujenga na Kukuza Maadili Mema kwenye Jamii-utafiti nilioufanya wilayani Kongwa." Walioshiriki kutoa maoni yao katika utafiti ule waligusia na umuhimu wa viongozi wa dini kuelimisha jamii kuishi maadili mema, kufanya maombi kwa ajili ya viongozi na taifa.

Aidha, viongozi wa dini kuwa vielelezo katika tabia njema, kukemea na kulaani vikali maovu katika jamii ili kuwa na taifa lenye maadili bora.

Kwa hiyo, viongozi wa dini waendelee kuelimisha waamini kuhusu utii wa sheria za Mungu na za nchi. Katika ibada wakumbuke kuiombea nchi na raia ili watu waache kutenda vitendo vya mauaji na ukatili.

Kukemea mauaji na ukatili ndani na nje ya nyumba za ibada kutasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya kikatili. Viongozi wa dini wasichoke kupaza sauti zao kwani vitendo vya aina hii ni chukizo mbele za Mungu na vinaharibu amani na utulivu ndani ya jamii. Viongozi wa dini wasisitize juu ya roho njema tulizoumbiwa na Mungu, hivyo roho za kikatili za mauaji na kikatili hazitokani na Mungu bali shetani, ambaye hatuna budi kumshinda kwa kutenda yale yampendezayo Mungu.

Kutokana na umuhimu wa viongozi wa dini katika kusaidia kufanikisha juhudi mbalimbali za kimaendeleo zinazofanywa na serikali, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa wilayani Ngara mkoani Kagera anawakumbusha hilo.

Alipohudhuria sherehe ya jubilei ya miaka 25 ya uaskofu wa Askofu wa Jimbo Katoliki la Rulenge-Ngara, Severine Niwemugizi, anawapa tena viongozi wa dini jukumu la kukemea mauaji nchini.

Rais Samia anaelezea namna anayokerwa na mauaji yanayoendelea nchini na kuwakumbusha kuwa kazi hiyo ni yao wasiikwepe.

Anataja matukio ya mauaji yanayotokana na watu kuuawa au kujiua akisema. "Askofu Niwemugizi umezungumzia suala zima la mmomonyoko wa maadili, ni kweli watu wako mbali na imani za dini zao, niwaombe sana turudi kwenye imani zetu, nitoe wito kwa viongozi wa dini turudi kwenye imani zetu watu wafuate misingi ya imani, sisi serikali tumeona tutaanza kuwafundisha watoto wetu shuleni maadili kwenye somo la uraia."

Kutokana na imani kubwa ya serikali kwa viongozi wa dini ni wakati wao wa kusimama katika nafasi zao kwa kusaidia kujenga jamii inayoheshimu sheria za Mungu na za nchi ili kuondokana na vitendo vya mauaji na ukatili.

**TANGAZO MAALUM**

# USHIRIKI WA TPA KATIKA MAONESHO YA DUBAI EXPO 2020

## MAKUBALIANO YA USHIRIKIANO YASAINIWA, TPA YAPATA DOLA MILIONI 500.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania TPA Bw Eric Hamissi na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya DPW ya Umoja wa Famle za Kiarabu, wakisani hati ya Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) ya kuendeleza Bandari za Tanzania.*

Kampuni ya Kimataifa ya Uchukuzi na lojistiki ya DPW ya Umoja wa Falme za Kiarabu itatumia dola za Kimarekani milioni 500 katika miradi mbalimbali iliyolenga kuboresha ufanisi katika bandari zinazomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Makubaliano ya kupatikana kwa fedha hizo yalitiwa saini katika maonesho ya biashara ya kimataifa ya Dubai (Dubai Export 2020) kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania TPA Bw Eric Hamissi na Mtendaji Mkuu wa wa DPW, Sultan Ahmed Bin Sulayem .

Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) yaliyofikiwa ni sehemu ya matukio muhimu wakati wa Ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Nchini Dubai ambapo alihudhuria Siku ya Tanzania katika maonesho hayo tarehe 26.02.2022.

Fedha zilizopatikana zitatumika kuendeleza Bandari za Tanzania kwa kuimarisha Mifumo ya TEHAMA, Mafunzo kwa Watumishi na Uendelezaji wa Miundombinu ya kibandari katika Bandari za Mwambao wa Bahari na Maziwa.

Fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya kuiwezesha Bandari ya Dar es Salaam kuongeza ushindani wake katika Viwango vya Kimataifa vya Ubora na Ufanisi wa Huduma.







*Matukio mbalimbali ya Wageni na Wadau waliotembelea Banda la TPA lililoko katika Banda la Tanzania katika Maonesho ya Expo Dubai 2020.*

# Serikali yashauriwa kuongeza kasi elimu chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imeshauriwa kuongeza kasi ya utoaji wa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19, kwa kushirikisha mashirika na taasisi binafsi ili jamii iachane na dhana potofu inayopinga chanjo hiyo.

Ushauri huo umetolewa na Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), ikifafanua kuwa, tangu ugonjwa huo kuingia nchini, kumekuwapo na elimu inayopotosha watu kuhusu chanjo na kwamba hali hiyo inaweza kuchangia watu wengi kutojitokeza kuchanjwa.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Thomas Ngawaiya, alisema, tangu chanjo ianze kutolewa Agosti mwaka jana, kuna sababu mbalimbali zimekuwa zikitolewa na baadhi ya watu wanaoipinga.

"Kwa mfano, tunawasikia baadhi ya watu wanadai kuwa hawaumwi au hawajawahi kupata corona, hivyo hawaoni ni kwa nini wakachanjwe, wengine hudai kuwa wana mashaka na ufanisi wa chanjo," alisema Ngawaiya.

Ngawaiya alisema, wengine wamekuwa wakidai kwamba chanjo ya UVIKO-19 imeletwa ili Watanzania wafanyiwe majaribio na sababu nyingine nyingi ambazo zinatokana na elimu waliofundishana mitaani.

"CEGODETA tunaamini kuwa dhana hizo ni potofu, ni vyema zikaondolewa vichwani mwa wale wanaoziamini, ili watu wengi zaidi wajitokeze kupata huduma hiyo kwa ajili ya usalama wa afya zao," alisema.

Alisema, ni muhimu kushirikisha kikamilifu mashirika na taasisi binafsi, kwa kuwa hayo ni miongoni mwa mwakundi yenye ushawishi katika jamii, na kwamba yanaweza kusaidia kutoa elimu sahihi kwa umma.

"Wadau hao wakishirikishwa kikamilifu kuhamasisha na kutoa elimu sahihi kuhusu chanjo, watu wengi wanaweza kujitokeza kupata huduma hiyo, hivyo wito wetu ni kwamba tushirikishwe na ikiwezekana litengwe fungu maalumu la kutuwezesha kufanya kazi hii," alisema.

Alisema jamii ikipata elimu sahihi, hakutakuwa na wanaodai kuwa chanjo inasababisha vifo, kuvuruga hedhi, kuharibu nguvu za uzazi kwa wanaume ama kushambulia mfumo wa vinasaba na kufanya watu kuwa 'mazombi'.

"Kwa kawaida mambo yanayopotosha huaminiwa haraka, ndiyo maana tunashauri elimu sahihi zaidi itolewe kwa wingi kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili kuhakikisha upotoshaji unakosa nafasi," alisema.

Alifafanua kuwa, kila Mtanzania ana uhuru wa kikatiba wa kutoa maoni au mawazo, na kwamba siyo upotoshaji kama ambao umejitokeza kwenye suala la chanjo na kusababisha sintofahamu kwenye jamii.

Hivi karibuni, Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe, alitoa taarifa kuwa, hadi kufikia Februari 6, mwaka huu, jumla ya watu 2,117,387, sawa na asilimia 3.67 walikuwa wamepata dozi kamili ya chanjo ya UVIKO-19.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (katikati), akionyesha kadi za benki ambazo mteja wa benki hiyo akitumia kwenye manunuzi ataingia kwenye droo ya MastaBata, ambapo jana droo ya mwezi ilichezeshwa jijini Dodoma. Kulia ni Ofisa Huduma kwa Wateja wa NMB, Suzan Manga na Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Ibrahim Shikana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Auawa kwa kuchomwa moto madai ya wizi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MTU aliyetambulika kwa jina moja la Sudi anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 24, mkazi wa Mtaa wa Nangaya Kata ya Migongo wilayani Masasi mkoani Mtwara, ameuawa kikatili kwa kupigwa na mchi, mawe kisha mwili wake kuchomwa moto na wananchi wenye hasira, kwa tuhuma za wizi wa vifaa vinavyotumia umeme ikiwamo televisheni.

Tukio hilo lilitokea mjini Masasi majira ya asubuhi, ambapo kijana huyo alikamatwa na wananchi hao kisha kumfanyia unyama huo, huku wakidai kuwa wamechoshwa na matukio ya mara kwa mara ya wizi yanayofanywa na kijana huyo.

Akizungumza na gazeti hili jana akiwa katika eneo la tukio hilo, Mtendaji wa Serikali ya Mtaa wa Nangaya, Majirani Joseph, alielezea kuwa ameshatoa taarifa za tukio hilo kituo kikuu cha polisi wilayani Masasi.

Alisema kijana huyo anadaiwa kuuawa kutokana na tuhuma za wizi wa vifaa vinavyotumia umeme kama televisheni na redio.

Joseph alisema kijana akiwa katika mizunguko yake ghafla alikutana na kundi la wananchi waliomkimbiza hadi walipofika katika mtaa wa Nangaya walifanikiwa kumkamta na kuanza kumpiga kwa kutumia silaha mbalimbali za jadi vikiwamo vitu vyenye ncha kali.

Alisema baada ya kupata majeraha makubwa, alipoteza maisha ndipo waliuchukua mwili kisha kumchoma moto na kumtupa katika moja ya nyumba moja ambayo haikaliwi na watu katika mtaa huo.

"Nilipofika eneo hili la tukio baada ya kupewa taarifa nilifika na kukuta ameshauawa na mwili wake kuchomwa moto," alisema.

Salama Hamisi, shuhuda, alisema aliona kundi la watu wakiwa wanampiga kijana huyo, na kwamba baada ya tukio hilo walitawanyika katika eneo hilo.

Ofisa wa polisi mkoani Mtwara ambaye hakutaka kutajwa jina lake gazetini alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa askari wao wilayani Masasi walishafika katika eneo la tukio.

## TBS yakabidhi leseni, vyeti kwa wazalishaji

**Na Joseph Mwendapole**

WAZALISHAJI wakubwa, wa kati na wajasiriamali 302 wamepatiwa vyeti na leseni za kutumia alama ya ubora ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) baadhi ya kukidhi vigezo kwa kipindi cha kuanzia Septemba hadi Desemba, mwaka jana ikiwa ni wastani wa vyeti 100 kila mwezi.

Hafla ya kukabidhi leseni na vyeti kwa wazalishaji ilifanyika makao makuu ya shirika hilo mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti hivyo, Kaimu Mkurugenzi wa TBS, Mhandisi Johanes Maganga, alisema kutokana na idadi ya vyeti la leseni iliyotolewa kuwa kubwa ni kielelezo kwamba kazi kubwa sana imefanyika na wazalishaji hao wamepata ufahamu mkubwa wa masuala ya ubora wa viwango.

Alisema katika leseni hizo, vyeti 163 sawa na asilimia 54 vimetolewa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, alisema shirika limetoa leseni na vyeti 139 sawa na asilimia 46 kwa wazalishaji wengine, vinahusisha bidhaa mbalimbali kama vile chakula, vipodozi, viatu, vifaa vya ujenzi, umeme, mitambo, magodoro, vibebeo pamoja na vifungashio.

"Vyote vimejumuishwa katika leseni ambazo zinatolewa. Kwa mafanikio haya natoa pongezi za dhati kwa Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kulipia gharama za kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati katika ukaguzi na upimaji wa bidhaa zao," alisema.

"Hii inaonyesha jinsi Rais Samia alivyo na imani na TBS, imani ambayo ndiyo msingi wa kuendelea kulijengea uwezo shirika katika maeneo mbalimbali ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu," alisema Maganga.

Alisema jitihada za serikali za kuimarisha uchumi kupitia sekta ya viwanda, shirika limeendelea kutenga bajeti ya kuwahudumia wajasiriamali wadogo kuanzia viwanda na kupata leseni ya kutumia alama ya ubora katika bidhaa.

Alitoa mfano kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Shirika limetenga Sh. milioni 256 kwa ajili ya kuwahudumia wajasiriamali wadogo ambao miongoni mwao walituni ukiwa vyeti na leseni mwishoni mwa wiki.

Alitoa wito kwa wajasiriamali kuchangamkia fursa hiyo inayotolewa na serikali kwa kuanzisha viwanda ili kuchangia kasi ya ukuaji wa uchumi nchini, kwa kuwa viwanda hivyo vinatengeneza ajira kwa Watanzania na serikali inapata kodi ambayo itatumika kuboresha huduma mbalimbali kwa wananchi.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora, Baraka Mbajije, alisema wazalishaji waliokabidhiwa vyeti na leseni ya kutumia alama ya ubora wamegawanyika katika makundi matatu, ambayo ni wazalishaji wakubwa, wa kati na wajasiriamali kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na wachache kutoka upande wa Zanzibar.

Alisema leseni na vyeti hivyo vitasaidia bidhaa zilizothibitishwa katika maeneo yafuatayo, moja kuongeza imani kwa umma wa Watanzania na hata wale walioko nje kwamba bidhaa zao ni salama na zinakidhi matakwa ya viwango na zinaweza kufanyakazi iliyokusudiwa na bidhaa husika.

## Madiwani sasa wataka elimu alama za mifugo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameishauri serikali kupitia idara ya mifugo kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa alama katika mifugo yao.

Wameitaka elimu hiyo kabla ya kuanza zoezi la kuweka mifugo alama za hereni ili kuleta ufanisi na tija katika utekelezaji wa agizo hilo.

Hayo yalibainisha na madiwani wa halmashauri hiyo katika kikao cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/23 kilichokuwa kinajadili taarifa mbalimbali za maendeleo, ikiwamo hali ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri hiyo.

Diwani wa Chambo, Daudi Mahona, alisema, wafugaji hawajaelimishwa kuhusiana na zoezi la kuweka alama katika mifugo yao hivyo ni budi serikali ikaweka utaratibu wa kukutana nao ili kuwaeleza kinaga ubaga kuhusiana na faida za kuweka alama za utambuzi kwenye mifugo yao hali itakayosaidia kuondokana na wizi.

"Sisi madiwani hatujapewa elimu juu ya umuhimu wa kuweka alama za utambuzi (hereni) ng'ombe, mbuzi na kondoo kama serikali inavyotaka, bei zake ziko juu ikilinganishwa na zoezi la awali ambapo walikuwa wanalipia Sh. 500 kwa ajili ya kuwekewa chapa,"alisema Mahona.

Naye Diwani wa Bukomela, Kulwa Shoto, aliiomba serikali kuwapunguzia wafugaji bei za kuweka hereni kwenye mifugo ambapo kwa sasa ng'ombe mmoja mfugaji analazimika kulipia Sh. 1,750 huku mbuzi na kondoo ikiwa ni Sh. 1,000, bei ambayo iko juu zaidi.

Alisema mwaka jana walikuwa wakiweka chapa kwenye mifugo kwa Sh. 500 kwa kila mfugo mmoja na ilileta shida kwa wafugaji na kushindwa kujitokeza zaidi na baadhi ya mifugo ilikufa kwa kuweka vibaya alama na sasa wanakuja na bei mpya kabla ya kuanza kutoa elimu juu ya umuhimu wa zoezi hilo.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema, busara inapaswa kuzingatiwa kabla ya kuanza utekelezaji wa zoezi hilo la kitaifa.

Awali akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mwalimu Linno Mwageni, alisema, serikali kupitia imetoa maelekezo juu ya uwekaji wa alama mpya za utambuzi wa mifugo ili kudhibiti vitendo vya wizi wa mifugo na upotevu wa mifugo mara kwa mara.

# Makundi maalum Kinondoni yakopeshwa bilioni 12/-

**Na Yasmine Protace**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam imekopesha Sh. 12,186,429,539 kwa vikundi 2,845 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kuanzia mwaka 2017 hadi 2022.

Hayo yalisemwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa hiyo, Zena Nalipa, alipokuwa akitoa mada katika semina ya Maendeleo na Jinsia (GDSS), inayoratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Alisema, manispaa hiyo imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ikiwamo kuwajengea uwezo na kuwainua kiuchumi wananchi wake kwa kuwapa mkopo unaotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani.

"Katika kufanikisha hilo, kuanzia mwaka 2017 hadi 2022, manispaa imeshatoa Sh. 12,186,429,539 za mkopo usio na riba kwa vikundi 2,845 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu," alisemwa Nalipa.

Alifafanua kuwa mwaka 2019/2020, manispaa ilikopesha Sh. 1,302,200,000 kwa vikundi 557 vya wanawake, Sh. 659,687,000 kwa vikundi 306 vya vijana na Sh.119,667,000 kwa vikundi 31 vya watu wenye ulemavu. "Manispaa ilitoa jumla ya Sh. 2,081,554,000 ambazo ziligawanywa kwenye makundi hayo matatu, ili yaweze kuinuka kiuchumi kwa kufanya biashara mbalimbali," alisema.

Nalipa aliendelea kufafanua kuwa mwaka 2021/2022, manispaa imekopesha Sh. 1,304,630 kwa vikundi 318 vya wanawake na Sh.1,053,077 kwa vikundi 68 vya vijana na Sh. 204,900,000 kwa vikundi 13 vya watu wenye ulemavu.

Aliongeza kuwa mpango mkakati wa manispaa hiyo ni kuboresha huduma za kijamii na kuimarisha uchumi kupitia malengo yake ambayo utekelezaji wake ni wa kipindi cha muda mrefu, wa kati na muda mfupi.

"Baadhi ya malengo hayo ni kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi, jinsia na ustawi wa jamii, kuimarika kwa utawala bora na utoaji wa huduma kwa jamii na kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma hizo," alisema. Aidha, alisema, manispaa hiyo pia hufanya shughuli za uwezeshaji wa kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na kwamba hadi Novemba mwaka jana, takriban kaya 3,070 za walengwa zimefikiwa.

"Manispaa pia imeunganisha vikundi vya wajasiriamali na fursa nyingine za kiuchumi kama maonyesho mbalimbali ya biashara yakiwamo ya Sabasaba, Nanenane na maadhimisho mbalimbali," alisema.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Ummy Wenceslaus, aliziomba manispaa kupanua wigo wa elimu kwa jamii ili watu wapate uelewa wa kutosha kuhusu mikopo inayotolewa kwa makundi hayo matatu wachangamkie fursa hiyo.

"Ninaamini kwamba kuna kundi kubwa la watu ambao hawaelewi kuwapo kwa mikopo hiyo, hivyo niwaombe mpanue wigo wa kutoa elimu ili watu wengi zaidi wajue na ikiwezekana wachangamkie fursa," alisema Ummy. Aliongeza kumekuwapo na tuhuma nyingi kuhusu mikopo hiyo, kwamba baadhi ya watumishi wasio waaminifu, kwa kushirikiana na wajanja wachache huitumia na kusababisha walengwa kukosa.



Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa, akimkabidhi cheti cha ushirikiano bora wa usalama barabarani, Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Amend, Saimon Kalolo (kulia), wakati wa uzinduzi wa mradi wa usalama barabarani kwa shule za msingi za serikali za jijini Dar es Salaam, ujulikanao 'Mahakama ya Watoto'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhaba wa vyoo waleta shida shuleni

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

SHULE ya Msingi Mseki iliyoko Kata ya Bulungwa, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, inakabiliwa na uhaba wa matundu ya vyoo, hali inayowapa shida wanafunzi hasa kipindi cha masika.

Shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 1,383 ina mahitaji ya vyoo 62, huku vilivyoko ni 11 na upungufu ni matundu 51, hali inayowapa usumbufu wanafunzi wakati wa mapumziko.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa shule hiyo, Robert Nteba, wakati wa harambee ya kusaidia ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa, ambavyo ujenzi wake unafadhiliwa na wafanyabiashara wa kata hiyo.

Alisema kuwa wakati wa kipindi cha masika wanafunzi hulazimika kujisaidia mashambani kutokana na vyoo vilivyoko.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, changamoto nyingine inayoikabili shule hiyo wanafunzi kutoka mbali ambao hutembea umbali mrefu.Aidha, alisema inapotokea matundu yamejaa wanalazimika kuwachangisha wanafunzi Sh. 500 kila mmoja kwa ajili ya kumlipa mtapishaji wakati wanaendelea na masomo.

Alikuwa akitoa taarifa kwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu, Emmanuely Makashi, aliyemwakilisha Mbunge wa Ushetu, Emmanuely Cherehani, kwenye harambee hiyo.

"Hali kwa ujumla katika shule hiyo si nzuri, tuliongea na wafanyabiashara wa kata hii kuona ni jinsi gani ya kuwasaidia wanafunzi hao, wamekubali na sasa watasaidia ujenzi huu," alisema.

Ofisa Elimu (Msingi) wa Halmashauri ya Ushetu, Velena Ntulo, alisema serikali imefurahishwa na uamuzi wa wafanyabiashara wa eneo hilo kujenga madarasa matatu na matundu hayo kwa nguvu zao, ili kusaidia maendeleo ya elimu wilayani humo. Aidha, alieleza kuwa uwepo wa wanafunzi wengi shuleni humo kunachangia utoro kwa kuwa walimu watashindwa kuwamudu hasa wanapokwenda vichakani kujisaidia.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara Kata ya Bulungwa, Michael Mbowe, alisema wanataka kuonyesha nguvu zao katika kujenga madarasa matatu katika shule hiyo ya msingi na waliwiwa kufanya hivyo.

Alisema madarasa hayo yakikamilika yatasaidia kwa kiasi kikubwa hata wanafunzi wanaoishi katika vijiji jirani kuhudhuria masomo yao kwa wakati na kuongeza harambee hiyo kwa kushirikiana na wafadhili itapunguza utoro.

Makamu Mwenyekiti Makashi, aliahidi kutenga fedha kwenye bajeti ijayo kwa kuwa kwa muda huu imeshawasilishwa serikani. Katika harambee hiyo zilipatikana Sh. milioni 2.3 na mifuko ya saruji 30.

# Wanahabari wapewa jukumu elimu ya UVIKO-19

**Na Neema Hussein,**
KATAVI

WAANDISHI wa habari mkoani Katavi wametakiwa kutumia taaluma yao kuwaelimisha wananchi kujitokeza kukamilisha dozi ya pili ya chanjo ya UVIKO -19. Akizungumza katika mafunzo ya siku moja yaliyoandaliwa kwa ajili ya waandishi wa habari na maofisa habari wa mkoa huo yaliyofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Mratibu wa chanjo mkoa wa Katavi, Stephano Kahindi, alisema mwitikio wa watu kupata dozi ya pili ni mdogo ikilinganishwa na mwitikio wa watu waliopata dozi ya kwanza.

Kahindi alisema lengo la mkoa ni kufikia Desemba mwaka huu wawe wamechanja watu 483,532 na hiyo ndio itakuwa asilimia 60 ya watu mkoa wa Katavi.

"Lakini mpaka kufikia Februari 8 tulikuwa tumeisha chanja watu 56,978, ukifanya hesabu ni sawa na asilimia 12 tu ya walengwa wa mkoa kwa hiyo utaona bado tuna asilimia ndogo sana ukilinganisha na lengo ambalo kama mkoa tumepewa na ili tupate kinga jamii inatakiwa angalau tufikishe asilimia 60 hapo ndio tutasema mdudu (kirusi) tutakuwa tumemdhibiti," alisema Kahindi.

Kahindi alisema pamoja na kuwa wamechanja watu 56, lakini bado kuna idadi kubwa ya watu ambao hawajapata dozi ya pili, na kusema watu 11,794 hawajapata dozi ya pili ya Pfizer na watu 10,461 hawajapata dozi ya pili ya Sinopharm.

"Tusipowapata hawa watu tutakuwa tumefanya kazi bure, hawa ni watu wengi, inahitaji tuwapate tuwakinge... kwa hiyo kwa ufupi nilitaka niwaeleze hayo nyie kama wataalamu wa magazeti, redio na Tv mkatusaidie kufikisha huu ujumbe," alisema Kahindi.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Dk. Thadeus Makwanda ambaye ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, alisema chanjo hazina madhara yoyote na mpaka sasa hakuna kesi yoyote ya mtu aliyedhurika na chanjo.

"Kwanini tunataka watu wengi wachanje, lengo letu ni kwamba ukitaka ugonjwa wowote wa mlipuko upotee, lazima zaidi ya watu asilimia 80 wawe wamechanja," aliongeza.

Mmoja wa waandishi wa habari, Irene Temu, alisema bado kuna baadhi ya watu wana imani potofu kuhusu chanjo ikiwamo hawatozaa tena na kutokuwa na nguvu za kiume, hivyo alishauri itafutwe njia mbadala ya kuondoa hizo imani potofu.




Ofisa Mkuu wa Tigo Pesa, Anjelica Pesha, akizungumza na wamiliki wa biashara mkoani Kilimanjaro juzi, wakati wa mkutano ulioandaliwa na kampuni ya Tigo, kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu huduma mpya zinazotolewa na kampuni hiyo, ikiwamo Tigo Pesa na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili ili kuzipatia ufumbuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri afunguka hatima ya mashambapori

**Na Christina Haule,** MOROGORO

NAIBU Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, amesema ataendelea kufanya mazungumzo na ofisi ya Hazina ili kuona sehemu ya mashambapori yaliyoko nchini inarudi kwa Ofisi ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) ili iyatumie katika kuongeza uzalishaji mbegu sambamba na kuwaongezea bajeti ya kuboresha kilimo.

Waziri huyo alisema hayo alipotembelea ofisi za ASA mkoani hapo ambapo alisema sambamba na mashamba 14 yaliyoko ni vema kuwaongezea mengine pamoja na bajeti ambapo pia ifahamike kuwa kilimo ni sayansi na kwamba hakuna uchawi wowote hivyo ili kumsaidia mkulima wa Tanzania ni lazima kuweka bajeti itakayosaidia kuwekeza katika sayansi.

Hivyo alisema sayansi inaanzia katika utafiti na uzalishaji wa mbegu bora na kinyume chake suala la kilimo halitapiga hatua nchini.

Alisema ASA, TOSCI na TARI ni taasisi muhimu ambazo zinapaswa kuwezeshwa kibajeti ili kufikia malengo ambapo watapunguza semina nyingi na mafunzo yaliyojaa Wizara ya Kilimo na kuwekeza katika bajeti kisayansi kwenye taasisi hizo ambazo zitasaidia kuleta tija kwa mkulima.

Hata hivyo, aliipongeza ASA kwa kuongeza uzalishaji wa mbegu kutoka tani 1,436 mwaka 2018 na sasa imefika mbali ambapo anaamini miaka ijayo watakuwa zaidi.

Alisema bado wana changamoto na kutakiwa kufikia malengo waliyojiwekea ya uzalishaji wa mbegu nchini na kufikia tani laki 3 ambapo kwa sasa wapo katika tani 7,500 zinazotoka ASA na kwa makampuni binafsi.

Naye kwake Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema wanakabiliwa na changamoto ya dhana za kufanya kazi, maghala ya kuhifadhia mbegu na miundombinu ya uzalishaji kwa sababu wanazalisha kwa kutumia mvua na inawapa changamoto hasa panapotokea changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema wana mashamba 14 katika ikolojia zote za uzalishaji nchini ambapo yapo baadhi ya mashamba yenye miundombinu mbalimbali ambayo inatumika.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, aliitaka ASA kuanzisha kilimo cha malisho ili kunusuru vifo vya mifugo vinavyotokana na ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

# Wadau wapendekeza mfumo kutunisha huduma afya pamoja

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa afya wakiwamo wabunge wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya, wameelezea umuhimu wa kuwapo mfumo maalum wa kutunisha Mfuko wa Huduma ya Afya ya Pamoja (UHC).UHC

Wakitoa maoni kwa nyakati tofauti kuhusu kuboreshwa kwa huduma ya afya nchini, wamesema kama ambavyo serikali ilivyoanzisha mfumo wa makato ya kodi kwa ajili ya kuchangia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), ufanyike pia kwa UHC.

Maoni hayo waliyatoa kwenye mafunzo yaliyoshirikisha washiriki 64 yaliyoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kupitia Mradi wa RECAP unaosimamiwa pia na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Mbunge wa Mbozi, George Mwanisongole, alisema jijini Dar es Salaam, kwenye mafunzo yaliyohusisha wajumbe wa hiyo pamoja na vyombo vya habari, kuwa ili kuwa na huduma ya afya ya pamoja iliyothabiti uwepo mjadala wa kitaifa ili kufikia mwafaka wa suala hilo.

"Huduma ya afya ya pamoja, UHC, ambayo inalenga kuhudumia Watanzania wote ili iwe thabiti inabidi tukubaliane kama taifa namna ya kuwa na mfumo wa uchangiaji endelevu.

"Niliwahi kufika Marekani nikapata uzoefu kwamba ili huduma ya afya iwe kwa wote, kila mmoja anachangia ingawa inaangalia kiwango cha pesa kwa kila mtu, kiasi gani anaingiza, ingawa huduma inapotolewa itahudumia wote kwa usawa bila," alisema Mwanisongole.

Dk. Waziri Ndonde alisema maandalizi yanahitajika ili kuhakikisha kinakuwapo chanzo cha pesa sahihi na cha muda mrefu ambacho kitawezesha huduma kupatikana ikiwamo vifaa, watoa huduma na vituo vya afya kuanzia ngazi ya kata.

"Tusiende haraka sana tujikite katika kupata suluhisho la pamoja na imara. UHC itakuwa bora zaidi na itamfikia kila mmoja iwapo kila mtu atakuwa tayari kuchangia," alisema Dk. Ndonde.

Mkurugenzi Msaidizi Magonjwa yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. James Kiologwe, alisema UHC itatoa fursa kwa Watanzania wote, na kwamba idadi ya wanaohudumiwa na bima ya afya ikiwamo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na za taasisi binafsi ni asilimia 33.

"UHC itawafikia wengi kwa kuwa hivi sasa NHIF inatoa huduma kwa asilimia 11 ya Watanzania, pia ipo CHF na bima zingine. Na Watanzania wengi wanapata huduma za afya kwa kulipia pesa taslimu jambo ambalo si salama kwa uchumi wa familia kwa sababu mmoja wa familia akiugua ugonjwa mkubwa baadhi huuza sehemu wa mali," alisema Dk. Kiologwe.


Nipashe
# TESA
Jumanne Machi 1, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12
Wasaidieni wenye mahitaji wasome



Ukurasa 13
Wadhalilishaji kijinsia kaeni mguu sawa



Ukurasa 14
**Profesa Kairuki anavyobakia kuwa alama ambayo wengi hawataisahau**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

AJABU KARNE YA 21

# Baba 'kuuza' mabinti, wakimaliza la saba anawaandalia wachumba

KUKUMBATIA mila na desturi kandamizi miongoni mwa wakazi wa Shinyanga kama kubagua watoto wa kike na kuwageuza vitega uchumi vya kujipatia mali na utajiri kama fedha na mifugo, ni janga sugu linalochochea mabinti kuozeshwa ndoa za utotoni na kukwamishwa kusoma.

Pengine ungeweza kusema Shinyanga si mahali salama kwa binti unapokisikia kisa cha binti aliyefaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu katika Shule ya Sekondari Pandagichiza wilayani Shinyanga (jina lake limehifadhiwa), aliyenusurika kuozwa kwa mahari ya ng'ombe 14.

Akiwa na miaka 15 pengine 'hajatosha' kuwa mama baba yake mzazi (jina tunalo) hakujali hilo, alimzuia kwenda kuanza masomo yake akitaka kumwozesha ili apate mali na mifugo, anazoondoka nazo kwenda mkoa jirani anapoishi.

Licha ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, kueleza kuwa mtoto ni yule mwenye umri chini ya miaka 18, ikilenga kuimarisha ulinzi na kutunzwa ikiwa ni pamoja na kupewa haki zote kuanzia chakula, malazi, mavazi, matibabu, pamoja na elimu bila ya kubagua jinsi yake.

Baadhi ya wazazi na walezi mkoani Shinyanga hawalizingatii hilo na huu ni ushuhuda wa kuendeleza ubaguzi kwa mtoto wa kike ambaye angekosa elimu, matunzo ya wazazi badala yake angeishia kuozwa utotoni.

**BABA ANATUKOMOA**

Nipashe baada ya kupata taarifa hiyo ilifunga safari hadi kijijini Sayu, Kata ya Pandagichiza kupata uhalisia wa tukio zima, habari ambayo inapochapishwa huenda ikaokoa wanafunzi wengi wa kike wanaokatishwa masomo na wazazi wao.

Anachoeleza binti ni kwamba baba yao amewatelekeza lakini akihakikisha kuwa anawaoza wanapomaliza darasa la saba, kukusanya ng'ombe na kwenda kuponda maisha.

Anaongeza kuwa baba yao, hajawahi kuwatunza aliwatelekeza tangu wadogo na yeye anatunzwa na familia nyingine ikiishi Tabora, lakini anachofanya ni kufuatilia kila wanapomaliza darasa la saba anakuja Tabora kuwaozesha kisha kuondoka na mifugo na mali anazopewa na waoaji.

Anasema ameshashuhudia dada zake wawili wakiozeshwa na baba yao ndoa za utotoni, na leo wana maisha magumu, kitendo ambacho kimemfanya kupata fundisho la athari za kuozeshwa katika umri ndogo bila kuwa na maarifa yoyote.

Anasimulia; "Baada ya baba kupata taarifa kuwa nimefaulu kuendelea na kidato cha kwanza, alikuja nyumbani na kunizuia kwenda shule, akisema kuwa amepanga kuniozesha, na tayari ameshaelewana na waoaji kuwa watampatia ng'ombe 14."

**AKIMBILIA KWA MTENDAJI**

Anasema baada ya kuambiwa kuwa anapaswa kuolewa na siyo kwenda kidato cha kwanza tena tayari mchumba ameshafika nyumbani kwao, hakufanya ajizi alitoroka kwa kuazima baiskeli kwa jirani, na kukimbilia hadi ofisi ya mtendaji kata zaidi ya kilomita 10, kutoa taarifa kuwa baba yake hataki asome bali kumwozesha.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Eliezer Feleshi, ofisi yake inawajibika kushughulikia marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu binti kuolewa. Mahakama ya Rufani iliagiza vipengele hivyo virekebishwe. **PICHA: MTANDAO**

"Mimi sitaki kuolewa nataka nisome nitimize ndoto zangu za kuwa mwalimu, ili nisaidie wadogo zangu na familia yangu ambayo baba ameitelekeza, nimeshuhudia maisha ya dada zangu walioozwa wakiwa wadogo wanavyosota sikuwa tayari,"anasema mwanafunzi huyo.

Anapofika ofisini, Mtendaji wa Kata ya Pandagichiza, Deogratius Mashamba, anasema baada ya kumpokea, anatoa taarifa dawati la jinsia la polisi ili wakamkamate baba yake, lakini alitoroka usiku wa manane na kukimbilia kusikojulikana lakini msako unaendelea.

Anasema awali mwanafunzi huyo walimpeleka kwenye Shirika la Agape, lakini baadaye ilibidi arudishwe nyumbani kwao ili aendelee na masomo na baada ya kuona hakuna usalama, kwani baba yake alidaiwa angeweza kumdhuru usiku au kumfanyia jambo baya kwa sababu alimtishia kumuua baada ya kugoma kuolewa, mama yake alimrudisha tena Agape.

Mama mzazi (jina lake tunalo), anasema mumewe alishamtelekeza, lakini anarudi kijijini humo kwa ajili ya kuozesha mabinti wake na kuondoka na mifugo yote anayolipwa akiwaacha patupu na kuendelea kukabiliwa na ugumu wa maisha.

Anasema anaungana na mtoto wake kukataa kuolewa, sababu haoni faida zaidi ya watoto wake kuteseka kwenye ndoa wakiwa na umri mdogo na kuiomba serikali imsaidie ili mtoto wake huyo asome akiamini kuwa atakuwa msaada kwa familia yao.

"Mume wangu alishaitelekeza familia na kwenda kuishi Tabora na mwanamke mwingine, na huyu mtoto anayetaka kumwozesha ni watatu sasa, lakini kutokana kupata elimu ya ukatili wa kijinsia, afya ya uzazi na umuhimu wa elimu kutoka kwenye mashirika, amemfumbua macho na kukataa kuolewa,"anasema mzazi.

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA NA KULWA MZEE

# WASAIDIENI WENYE MAHITAJI WASOME

KUTOKANA na changamoto mbalimbali katika familia ikiwamo vifo vya wazazi, baba na mama kutengana, kutelekeza watoto na hata kutupa watoto wachanga kumesababisha kuwa na watoto wengine wengi wanaohitaji msaada.

Hali hiyo inasababisha watoto wengi kuishi mitaani na sababu nyingi zikichangia kujikuta katika mazingira hayo. Kila mtoto ana hadithi yake, kuhusu changamoto zilizowafanya kujiingiza mitaani. Visa vyao vinatofautiana kutoka kwa familia moja na nyingine kama umaskini, kuhama makazi yao kwa sababu ya majanga ya asili na mizozo au kuvunjika kwa familia kwani yote husababisha kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Umaskini wa kiuchumi una nafasi kubwa ya kusababisha madhila hayo lakini kuna sababu nyingine kama vifo vya wazazi au kupuuzwa kwa wazazi na mambo mengine ya kijamii kama vile unyanyasaji wa watoto nyumbani au katika jamii.

Watoto wanaweza kuhamia mitaani na kuishi mazingira magumu kwa sababu nyingine ikiwamo kulazimishwa kufanya shughuli za uhalifu na kukataliwa na familia zao.

Kuwapo kwa wimbi kubwa la watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu kunaifanya serikali kuruhusu kuwapo vituo vya kulea watoto hao pamoja na kuwapa haki zote za msingi kama elimu bora.

Vituo viko vingi kimojawapo ni cha kusaidia yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Msongola Orphanage Trust Fund kilichoko jijini Dar es Salaam, chenye watoto 41 wakiwamo wa kike 20 na kiume 21.

Mama mlezi wa watoto hao, Christina Haule, anasema kinatunza watoto wenye umri kuanzia mwaka mmoja na nusu na kuendelea, lakini wapo wanafunzi kuanzia shule ya chekechea hadi sekondari wanaoishi katika kituo hicho, wanaofikishwa kwao na Ustawi wa Jamii.




Choo cha wahitaji kama kinavyoonekana. **PICHA : KULWA MZEE**

> “Ustawi wa Jamii wanatuletea watoto wenye matatizo mbalimbali wakiwa na nyaraka zinazowatambulisha lakini asilimia kubwa ni yatima.

Christina anaeleza kuwa shule wanazosoma watoto hao ni Shule za Msingi Msongola na Yangeyange na za sekondari ni Hilali na Msongola na nyingine zilizoko maeneo jirani na kituo.

“Ustawi wa Jamii wanatuletea watoto wenye matatizo mbalimbali wakiwa na nyaraka zinazowatambulisha lakini asilimia kubwa ni yatima. Wengine wana wazazi mmoja mwingine alifariki aliyebakia hana uwezo. Serikali ikipata taarifa ya watoto wanaishi maisha magumu inaingilia kati,” anasema Christina.

Aidha, anaongeza kuwa katika kituo hicho kuna kisa cha binti aliyekuja Dar es Salaam kwa ahadi ya kufanya kazi za ndani lakini mwenye nyumba akataka kumbaka kwa kumlazimisha kufanya naye ngono akaamua kutoroka na kufikishwa kituoni hapo.

“Huyu mtoto alipobainika anateseka aliletwa kituoni na Ustawi wa Jamii Msongola. Nisema watoto wana matukio mengi yaliyowakimbiza nyumbani kwa walezi, wapo waliokuwa wanapigwa na hata kukatwa vidole.”

### ANAELEZA CHANGAMOTO

Akizungumzia matatizo yanayowakwamisha kituoni hapo anataja kuni za kupikia chakula hakuna na zinazopatikana hazitoshi, umeme kwa ajili ya kusukuma pampu za maji, chakula kama maharage yanayowafikia hayawatoshelezi kwani kwa siku wanapika kilo sita mpaka saba za maharage.

Anasema changamoto nyingine ni mafuta ya kula, jengo wanalolitumia ni moja, vyoo havitoshi viko viwili kimoja kwa ajili ya watoto wa kike na kingine ni cha wavulana. Anataja mabegi ya kuhifadhia nguo, vitanda na kwamba baadhi wanalala chini hivyo kuomba wapatiwe misaada.

Mama mlezi anawageukia wamiliki wa shule mbalimbali za sekondari kukubali kupokea watoto wanaotoka katika kituo hicho kwani hadi sasa shule binafsi zinazowasaidia ni chache, ya msingi ni Zawadi wakati sekondari ni ya Mbonea.

Mlezi wa kituo hicho, Zakaria Maloba anasema anafanya kazi ya kujitolea, kituo kinapata msaada kutoka kwa wasamaria wema na kwamba kilianzishwa mwaka 2004 na rasmi kilianza kazi 2006, lakini hawajapata usajili wa makazi.

Mama wa Ustawi wa Jamii Msongola anatutembelea kila wakati, awali tulianza tukiwa na watoto 10 na sasa tunao 41, ambao walishamaliza shule wako kazini na wengine kidato cha sita.

Anaeleza kuwa wanahitaji wasamaria wema kuendelea kuwapa misaada mbalimbali na wamekuwa wakiipata kutoka sehemu mbalimbali, akisema baadhi ya waliofika kutoa misaada ni Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto, aliywapatia magodoro na vyandarua kadhaa.

Anawataja pia baadhi ya wanachama wa CCM walitoa misaada na Shule ya Msingi Zawadi iliyokisaidia vifaa vya kusomea, vitabu, madaftari, sabuni za kufulia na nguo, akisema misaada ya nguo za kike ndiyo mingi kuliko nguo za watoto wa kiume, akiwaomba Watanzania kujitoa kwa hali na mali kusaidia watoto hao na wengine wengi wahitaji ili

## Baba ‘kuuza’ mabinti wasisome, huandaa wachumba wakimaliza shule

**INATOKA UK.11**

“Namuunga mkono mtoto wangu kugoma kuolewa, na ndiyo maana ilibidi nimtoke hapa nyumbani na kumpeleka kwenye Shirika la Agape huko mjini Shinyanga, ambalo lina nyumba salama ya walionusurika na ndoa za utotoni, ili akaishi na kusoma huko sababu hapa nyumbani siyo salama, baba yake anaweza kumfanyia lolote,” anaongeza.

### KUINGIA SHULENI

Mkuu wa Sekondari ya Pandagichiza, George Vangilisasi, anakiri kuwa binti huyo alindikishwa shuleni hapo, lakini tangu usajili hawajawahi kuonekana akibainisha kuwa shule hiyo itapokea wanafunzi 172 wa kidato cha kwanza, lakini walioripoti shule ni wanafunzi 88, wavulana 51, wasichana 37.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, anazungumzia kupokelewa mwanafunzi huyo kwa mara ya pili, awali alipelekwa na mtendaji wa Kata ya Pandagichiza Deogratius Mashamba, na awamu ya pili mama yake mzazi, akidai kuwa mtoto wake hayupo salama huko kijijini.

Anasema, kutokana na maelezo ya mama na mazingira ya mtoto huyo aliyonayo ilibidi wampokee na sasa anaandaliwa kupelekwa Sekondari ya Mwangulumbi iliyoko Manispaa ya Shinyanga, jirani na nyumba yao salama ya kuhifadhi watoto wenye changamoto za mimba na ndoa za utotoni.

Anasema kwa mwaka huu ndani ya mwezi mmoja, tayari wameshapokea watoto saba ambao wamekumbana na mikasa ya kutaka kuozeshwa ndoa za utotoni na wazazi au walezi wao na kubainisha kuwa changamoto kubwa ambayo inawakabili kwa sasa kwenye nyumba hiyo salama, ni upungufu wa chakula na fedha za kuwatimizia mahitaji muhimu.

Mkuu wa Dawati la Jinsia la Polisi wilayani Shinyanga, Brighton Rutajama, anasema wana taarifa zake na wamesha mfungulia baba yake kesi ya jinai sababu alimtishia kumuua mtoto wake kutokana na kugoma kuolewa na sasa anatafutwa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omari, anakemea vitendo vya baadhi ya wazazi mkoani humo kuendekeza tabia ya kukatisha masomo watoto wao na kuwaozesha ndoa za utotoni na kubainisha wataendelea kuwachukulia hatua za kisheria.

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Wadhalilishaji kijinsia mguu sawa

## • UNFPA, polisi kukomesha maeneo vinara

WATOTO wa kike wanakwamishwa kielimu na mambo mengi, ukatili wa kijinsia kama ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni, kubaguliwa wanaume wakipewa kipaumbele huchangia kukatisha hatima zao kielimu.

Katika kukabiliana na vitendo hivyo, serikali kwa kushirikiana na wadau inafanya jitihada mbalimbali ikiwamo kutoa elimu ili kuvikomesha, kwani kimsingi vinatokana na mila zilizopitwa na wakati.

Mambo hayo yanaliibua Jeshi la Polisi kuanzisha Dawati ya Jinsia na Watoto linaloshughulikia na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji watoto, lakini na vitendo vyote vya udhalilishaji wa makundi yote.

Katika kuongeza msukumo kwenye vita dhidi ya vitendo vya ukatili, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Tanzania, linatoa pikipiki 10 kwa jeshi hilo ili kufanikisha operesheni ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Pikipiki hizo zenye thamani ya Shilingi milioni 51.3 zinakabidhiwa kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi IGP Simon Sirro na mwakilishi wa shirika hilo, Georgette Kyomba, jijini Dar es Salaam, hivi karibuni.



Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, akijaribu moja ya pikipiki ambazo jeshi hilo limepewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA). Kulia ni mwakilishi wa shirika hilo nchini, Georgette Kyomba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akipokea msaada huo, IGP Sirro anasema, zitawawezesha maofisa wa polisi walioko kwenye madawati ya jinsia ya watoto kuifikia jamii na kutoa elimu itakayofanikisha kuondoa na hata kupunguza vitendo hivyo.

Anaongeza kuwa pikipiki hizo pia zitaongeza wigo wa madawati hayo katika kuwafikia waathiriwa wa matukio ya ukatili wa kijinsia katika maeneo ambayo msaada umeelekezwa.

"Jambo la msingi ni kwamba, jamii iachane na mila potofu na pia tunahitaji juhudi za pamoja katika kukomesha vitendo vya ukatili wa kijinsia na ninaamini, huu utawawezesha maofisa walioko katika madawati kuifikia jamii kirahisi na kutoa elimu," IGP Sirro anaongeza.

Aidha, IGP Sirro anaiomba UNFPA kuangalia uwezekano wa kuwasaidia polisi kwenye ngazi za kata, kama njia ya kuongeza kasi ya kupatikana taarifa, kwa maelezo kwamba huko ndiko kwenye matukio mengi zaidi.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, anasema, amekabidhiwa pikipiki hizo ili zikatumike katika wilaya za Bunda, Butiama, Serengeti mkoani Mara na Buhigwe, Manyovu, Uvinza katika Mkoa wa Kigoma.

> Wale wanaokubali na kuachana na vitendo hivyo kuwachukua watoto wao na kuwaacha waendelee na masomo ili kutimiza ndoto walizojiwekea katika elimu.

Mwakilishi wa UNFPA, Georgette, anasema, Tanzania kama yalivyo mataifa mengine inakabiliwa na matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake, akifafanua kuwa katika visa 10, wanawake walio na umri wa kati ya miaka 15 hadi 49, hukumbana na ukatili huo.

"Msaada huu unalenga kumlinda msichana, mwanamke na mzee dhidi ya vitendo vya kikatili ikiwamo ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni , kuuliwa kwa tuhuma za uchawi, kupigwa na kufukuzwa kwenye jamii ili kufikia malengo ya mpango wa taifa wa kupinga ukatili," anasema Kyomba.

Kyomba anasema, asilimia 58 ya wanawake waliofanyiwa ukeketaji wapo mkoani Manyara, ikizidi kiwango cha kitaifa ambacho ni asilimia 10, na kwamba kasi ya kutokomeza vitendo hivyo inahitajika.

"Ukifuatilia kwa umakini, utabaini kuwa, katika matukio hayo, wamo waliojeruhiwa, familia kuvunjika moyo, jamii na kusababisha kushuka kwa uchumi miongoni mwa jamii," anasema.

Anafafanua kuwa, ukeketaji, ndoa za utotoni, mimba na ukatili wa aina nyingine vinasababisha ulemavu, vifo na matatizo ya kisaikolojia na kumfanya mtendewa kutofikia maendeleo aliyojiwekea.

Anasema, wana mkakati wa kufungua madawati matatu mapya ya kijinsia mkoani Manyara na kufanyia ukarabati dawati la Msalala mkoani Shinyanga na kuwajengea uwezo maofisa wa polisi kwa kuwapa mafunzo yanayohusu madawati hayo ili katika utendaji wao, wawe wanatoa msaada kwa wakati.

"Matarajio yetu ni kwamba, kwa kutumia pikipiki tulizotoa, waathiriwa wa matukio ya ukatili wa kijinsia watatambuliwa haraka, kulindwa na kusaidiwa na kuondoa ukimya unatokana na mila potofu kuhusu matukio hayo," anasema.

Wilaya ya Serengeti mkoani Mara, ni miongoni mwa zile zenye ripoti za juu za vitendo vya ukatili wa kijinsia, ukeketaji ambavyo husababisha baadhi ya wanafunzi kukimbia nyumbani kuepuka kuumizwa.

Wengine hukumbilia kituo cha Nyumba Salama kilichoko mjini Mugumu na kuhifadhiwa na Shirika la Hope for Girls and Women Tanzania ambalo Mkurugenzi wake ni Rhobi Samwelly, analiambia gazeti hili kuwa, Desemba kila mwaka shirika lake hupokea wanafunzi wengi wa kike wanaokimbia nyumbani kwao kuepuka kukeketwa na kuwahifadhi katika kituo cha Nyumba Salama.

Anasema kituo hulazimika kuwatafutia shule eneo la jirani ili waendelee na masomo, kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi mbalimbali katika jamii, wakiwafuata wazazi na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji.

Katika utoaji wa elimu hiyo, anasema, wale wanaokubali na kuachana na vitendo hivyo kuwachukua watoto wao na kuwaacha waendelee na masomo ili kutimiza ndoto walizojiwekea katika elimu.

Anafafanua kuwa wazazi au walezi wasiokubali kuachana na mila hizo, shirika hilo linaviachia vyombo vya dola huku watoto wao wakiendelea na shule wakiwa katika kituo cha Nyumba Salama.

ELIMU

NA JOSEPH MWENDAPOLE

# Profesa Kairuki anavyobakia kuwa alama ambayo wengi hawataisahau

PROFESA Hubert Kairuki, alikuwa mtu wa maneno machache, lakini mwenye matendo makubwa. Kuingia kwake kwenye sekta ya afya na tiba hadi alipofariki 1999, kumeacha kazi nyingi.

Hospitali, vituo vya afya vilivyojengwa kwa maono yake ni alama zinazoonyesha kuwa wengi wanazitumia kunufaika, wanaendelea kutafakari, kuiga ujasiri na uthubutu aliokuwa nao daktari huyo bingwa.

Amefariki miaka 23 iliyopita lakini ameacha alama zinazoishi. Ni Februari mwaka huu yamefanyika maadhimisho ya miaka 23 ya kumbukizi za kifo chake.

Ni katika kituo cha Kairuki Polyclinic Mbezi Terminal, kilichomuenzi kwa kutoa huduma mbalimbali za afya bila malipo kusherehekea maisha ya kujali watu aliyoyaishi.

Msomi huyo aliaga dunia mwaka 1999 na kuhifadhiwa kwenye hospitali aliyoianzisha ya Kairuki Hospitali iliyoko Mikocheni Dar es Salaam.

Ni daktari wa binadamu mzawa aliyeacha alama zinazoishi kwenye sekta ya afya nchini.

Ameanzisha hospitali ya kwanza binafsi wakati huo ikiwa vigumu serikali kuruhusu huduma hizo kutolewa na sekta binafsi, lakini kutokana na umahiri wake Profesa Kairuki aliweza kuishawishi serikali na kutimiza lengo lake la kuanzisha Hospitali ya Mikocheni.

Profesa Kairuki hakuishia hapo ni mwanzilishi wa Mtandao wa Afya na Elimu (KHEN), ambao umeanzisha Chuo cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), kilichoanza kazi tangu 1997.

Mbali na kuanzishwa kwa chuo hicho kikuu, KHEN pia imeanzisha Chuo cha Uuguzi Kairuki (KSN), ambavyo kwa pamoja vimeendelea kutoa huduma mbalimbali, zilizokuwa maono yake.

Mwenyekiti wa KHEN, Kokushubila Kairuki, anazungumza na Nipashe, akisema tangu muasisi wa mtandao huo alipofariki wamekuwa wakiongozwa na fikra zake katika kutoa huduma za afya kwa wateja wao.

Aidha, kwa upande wa hospitali wamehakikisha kuwa hospitali inasimama na kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

"Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki na kile cha Uuguzi cha Kairuki, tumeendelea kufundisha madaktari na wauguzi mahiri ambao kufikia mwisho wa mwaka jana tumefikisha idadi ya wahitimu madaktari wa shahada ya kwanza 1,512 na mabingwa ni 63, wakati wauguzi ni 1,205, washauri nasaha 205. Hawa wanatoa huduma katika hospitali mbalimbali za umma na binafsi," anasema.



Kutibu wakubwa kwa wadogo na kueneza elimu ya afya kwa wote ni moja ya maono ya Profesa Kairuki, yanayotekelezwa na taasisi alizoanzisha licha ya kuondoka. **PICHA: MTANDAO**

> Programu hizo ni pamoja na elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio na TV, kusaidia vituo vya watoto yatima, programu ya elimu ya afya ya uzazi katika maeneo ya Mikocheni na Boko.

Kokushubila anaongeza kuwa Chuo cha HKMU kimetoa wahitimu wa shahada za uzamili wa Sayansi ya Afya ya Jamii 24 na wengine wa Ustawi wa Jamii 41 wanatoa huduma za kitaalamu katika mashirika mbalimbali.

Anaeleza KHEN inaendelea na juhudi za kuisaidia jamii kuwa na afya njema, kwa kupitia programu mbalimbali za kusaidia jamii ambazo wamekuwa wakizifanya katika kipindi cha miaka 35 tangu ilipoanzishwa Kairuki Hospitali.

"Programu hizo ni pamoja na elimu kwa umma kupitia vipindi vya redio na TV, kusaidia vituo vya watoto yatima, programu ya elimu ya afya ya uzazi katika maeneo ya Mikocheni na Boko," anaeleza Kokushubila.

Aidha, kuna programu za kutoa huduma ya kwanza bila malipo kwa Shule ya Msingi ya Mikocheni.

Kokushubila anasema katika kumuenzi hayati Profesa Kairuki kwa vitendo, mwaka huu wametoa huduma mbalimbali za afya kwa wananchi bila malipo.

Anazitaja kuwa ni pamoja na uchunguzi wa awali wa saratani ya matiti, upimaji wa saratani ya tezi dume kwa kutumia ultrasound, kupima macho, shinikizo la damu (BP), uwiano wa uzito na urefu (BMI) na kutoa ushauri wa kitabibu kwa wananchi.

Kilele cha maadhimisho hayo kinakamilishwa na Mganga Mkuu wa Manispaa ya Ubungo, Dk. Peter Msanya, anayesema ikiwa imepita miaka 23 tangu mwasisi huyo kufariki ni fahari kuona wanaendelea kutenda yale aliyokuwa akiyafanya katika kuwahudumia Watanzania.

Anawapongeza kwa kutoa huduma ya afya na ushauri kwa wananchi bila malipo ikiwa ni namna ya kukumbuka maisha ya mwasisi Profesa Kairuki.

"Hatua mliyochukua ya kuanzisha kituo kipya cha huduma ya afya cha Kairuki Polyclinic mlichofungua hapa katika kituo cha mabasi cha Mbezi ili kuwasogezea huduma ya afya wananchi wa Mbezi Luis pamoja na Watanzania kwa ujumla kwani hata wasafiri wanaweza kupata huduma ya afya kwa haraka pindi watakapohitaji. Hii ni hatua kubwa sana kwa taasisi yenu na uwe mfano wa kuigwa," anasema.

Anasema kupima afya mara kwa mara ni utamaduni unaozoeleka nchi zilizoendelea kuliko Tanzania na kwamba hali hiyo imesababishwa na changamoto za upatikanaji wa huduma za afya na pia mazoea ya watu wengi kupima wanapougua.

"Pamoja na hayo na kukipongeza kituo chenu kwa kutoa huduma hizi za afya bila malipo na kuwapa wananchi elimu pamoja na ushauri wa kitabibu unaosaidia kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kupima afya zao ili kufahamu magonjwa mbalimbali na namna ya kujikinga," anasema Msanya.

"Nimesikia ushauri wa kitabibu kuwa uwiano kati ya uzito na urefu yaani 'body mass index' na shinikizo la damu vinatokana na mfumo wa maisha na aina za vyakula tunavyokula. Tunaweza kupunguza idadi ya wagonjwa wa moyo kama tukizingatia ushauri wa wataalamu wa afya," Msanya anasema.

Anauomba uongozi wa Taasisi za Kairuki uendelee kusaidia jamii ili iwe na afya njema na taarifa sahihi za magonjwa na namna ya kujikinga na maradhi mbalimbali.

"Nawaomba sana mwendelee kusogeza huduma kwa wananchi wengi zaidi kama mlivyofanya hapa Kairuki Polyclinic na mfikirie kuanzisha vituo vipya vya huduma ya afya hata nje ya Dar es Salaam ikiwa ni mwendelezo wa maono ya mwasisi na kutunza historia ya mzalendo mahiri, Profesa Hubert Kairuki," anaongeza Mganga Mkuu Msanya.

"Ninatoa wito kwa taasisi nyingine za afya hasa zile za binafsi kuungana na Jumuiya ya Mtandao wa Afya na Elimu wa Kairuki KHEN katika jukumu hili la msingi la kuhudumia jamii."



# Jimuiya Maridhiano yahamasisha taasisi uchangiaji wa damu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Maridhiano, Mkoa wa Dodoma, Askofu Dk. Evance Chande, ameziomba taasisi, mashirika na watu binafsi kujitokeza kuchangia damu ili kuwasaidia kuokoa maisha ya watu wenye uhitaji na huduma hiyo.

Dk. Chande alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye uchangiaji damu uliofanyika kwenye kituo kidogo cha damu salama Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema uchangiaji huo uliowahusisha wanachama na viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Maaridhiano itakayofanyika Machi 3, mwaka huu.

Alisema kuwa bado kuna makundi makubwa ya jamii yanayohitaji kuchangiwa damu hiyo kama vile kwa watoto na kinamama na kuwataka kujitoa ili hospitali, vituo vya afya na zahanati ziwe na akiba ya damu.

"Sisi wana maaridhiano mkoa wa Dodoma tumeamua tunapoelekea kuhadhimisha Siku ya Maridhiano, kuchangia damu kwenye hospitali yetu hii ili iweze kuwasaidia watu wenye mahitaji," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Wilaya ya Chamwino, Pili Yomba, alishauri wanawake kujitokeza kwa wingi kwenye kutoa damu kwa kuwa wao ndio wenye uhitaji mkubwa pindi wanapoumwa.

Alisema kuwa damu pamoja kuwa inahusika kwa kila mgonjwa, lakini wanawake na watoto ndiyo wahusika wakubwa wanaohudumiwa zaidi kutokana na magonjwa wanayokabiliana nayo.

Kwa upande wake, mtaalamu wa maabara Kanda ya Kati, Sulbesto Nicholaus, alisema mahitaji ya damu bado ni tatizo kubwa kutokana na kuwa na wagonjwa wengi wanaohitaji.

"Kwa siku lazima tuwapatie wagonjwa 10 hadi 15 damu, hivyo mahitaji bado yanahitajika kwa wingi ili tuweze kuwahudumia wagonjwa ambao wana shida ya kuongezewa damu hivyo, hivyo basi nitoe shukrani zangu kwa Jumuiya ya Maridhiano kutokana na mchango mkubwa wa kujitolea damu na ninaomba taasisi na mashirika kuiga mfano huu,"alisema.,

# Wito udhibiti ukatili wa kijinsia mitandaoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, amesema kuna ukatili mkubwa unafanywa mitandaoni na kushauri katika Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ujao utambue ukatili huo ili ushughulikiwe.

Lugangira aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo kwenye kikao cha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na wadau wanaotekeleza afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

"Wakati umefika sasa MTAKUWWA itambue ukatili wa kijinsia unaofanywa mitandaoni kwa sababu kuna ukatili mkubwa sana unaofanya mitandaoni," alisema.

Alieleza kuwa wakati MTAKUWWA inaandikwa bado ushirikishwaji na matumizi ya mitandao ya jamii yalikuwa hayajashamiri.

"Hivi sasa kuna ukatili mkubwa sana mitandaoni kwa watoto wa kike, wanawake wafanyabiashara, wanawake viongozi na hata sisi wabunge wanawake ni hatari naomba nipendekeze tuangalie ni kwa namna gani tutaongeze suala la ukatili wa kijinsia mitandaoni katika moja ya vitu ambavyo MTAKUWWA itakuwa inaangazia," alisema.

Aidha, alisema mwaka jana alifanya tathmini kupitia ofisi yake iliyoko Mkoa wa Kagera kuangalia hali ya ukatili wa kijinsia kwa mkoani humo na kubaini elimu ya ukatili wa kijinsia bado haijafika kwa jamii.

"Kule chini bado watu hawajajua jinsi ya kujikinga, kushtaki, lakini madawati ya kijinsia yapo kituo cha polisi kwa hiyo hata mtu akiwa anataka kwenda anapata hofu ya kuingia ndani ya kituo, kuna kuwa na kichumba ndani ya kituo lakini kichumba kile anakuwa hapati privacy kwa hiyo tunaweza kuangalia namna gani tunavyoweza kufanya madawati haya yasiwe ndani ya kituo cha polisi," alisema. Akizungumzia suala la afya ya akili, mbunge huyo alisema matukio mengi ya ukatili yanayoendelea kutokea yanahitaji afya ya akili.

"Wizara hii kwa kushirikiana na wadau tuone namna gani tutaweza ili Watanzania waone ni kawaida kwenda kuongeza na mshauri nasaha, kwenye shule zetu wawepo hawa wataalam, ifike mahala isiwe ajabu mtu kwenda kuongea au mtu yeyote ambaye amesomea suala husika ili aweze kupunguza au kukabiliana na msongo wa mawazo," alisema.

Alisema matukio yanayotokea mengi ni kutokana na msongo wa mawazo ambayo yanahitaji afya ya akili.

"Wakati umefika wa kutambua tuna changamoto kubwa na tukabiliane na hali hii, tupo tayari kuhakikisha wizara hii inafanya vizuri na tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha wizara hii maalum," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabirm Shekimweri (katikati), akikata utepe ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa anwani za makazi katika Mtaa wa Swaswa Ng'ambo Kata ya Ipaga, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 7.9/- kujenga soko la kisasa la machinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetenga Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa la wafanyabiashara ndogo (Machinga Open Market) litakalokuwa likifanya kazi kwa saa 24.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema kuwa ujenzi wa soko hilo lililoko eneo ya Bahi Road jijini hapa litakapokamilika wanatarajia kumkabidhi Rais Samia Suluhu Hassan Machi 17, mwaka huu, ikiwa ni zawadi yake kwake tangu aingie madarakani.

Mafuru alisema kuwa pamoja na kumkabidhi Rais Samia soko hilo kama zawadi kwa upande wa Halmashauri ya Jiji ni utekelezaji wa mipango wake wa mikakati ya kuwawekea miundombinu rafiki wamachinga ili kufanya biashara kwenye mazingira ya uhakika na salama.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa ujenzi wa soko hilo litakalokuwa na biashara za aina mbalimbali umekamilika kwa kiwango cha asilimia 70.

Alisema kuwa mradi huo ni wa kisasa utakuwa na huduma zote za kijamii ikiwamo huduma ya nyama choma siku zote kwa saa 24, vinywaji, mafundi viatu na kupaka rangi viatu, wapaka urembo kucha na huduma zote muhimu za kibinadamu.

Alibainisha kuwa baada ya kukabidhiwa kwa Rais, kuanzia Machi 18 wafanyabiashara wote watakuwa wameondolewa mitaani na maeneo yasiyo rasmi kwa biashara ili kuanza kulitumia soko hilo.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ambapo awamu ya kwanza ya mradi huo imegharimu Sh. bilioni 4.9 na mpaka sasa wameshalipa mkandarasi Sh. bilioni tatu huku mradi mzima ukigharimu Sh.bilioni 7.9.

Alisema soko hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara 5,000, lakini kwa takwimu walizonazo hivi sasa machinga hawazidi 3,000.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa machinga walishirikishwa katika kila hatua za utekelezaji wa mradi huo, na mpaka sasa hakuna tatizo lolote walilopata katika kuutekeleza kwa kuwa fedha zipo zinasubiri utendaji wa kazi tu.

"Tutahakikisha tunaandaa kanzi data ambayo itawatambua machinga wote na tutahakikisha hakuna mamluki katika kazi hii, litakuwa soko la kisasa na tutakuwa tumemaliza tatizo la machinga mkoa mzima maana wote wataingia hapa," alisisitiza.



# Wakulima maparachichi wawezeshwa

Na Nebart Msokwa, RUNGWE

SHIRIKA moja lisilo la kiserikali limewawezesha wakulima wadogo wa maparachini wilayani Rungwe kwa kuwapatia vifaa, baada ya kubaini wakitumia vifaa duni.

Wakulima hao wa maparachichi wanavuna matunda yao kwa kutumia njia za kienyeji ikiwamo kupiga na fimbo na kutikisa hali ambayo inadaiwa kupunguza ubora na kusababisha wanunuzi kununua kwa bei ndogo.

Vilevile wanadaiwa kuhifadhi matunda yao kwenye vifaa vya kienyeji ikiwamo magunia na vikapu, hali ambayo inasababisha matunda hayo kuharibika kabla hayajawafikia wanunuzi, hivyo kuwasababishia hasara.

Mkurugenzi wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la HELVETAS-KIBOWAVI, Daniel Kalimbiya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati shirika hilo lilipokuwa linakabidhi makreti 800 ya kuvunia maparachichi yenye thamani ya Sh. milioni 14.4 kwa Chama cha Wakulima wa Maparachichi Rungwe (UWAMARU AMCOS).

Kalimbya alisema njia hizo za kienyeji za uvunaji wa maparachichi husababisha matunda kupasuka na hivyo kukataliwa na wanunuzi ama kununuliwa kwa bei ya chini.

Alisema ili kuwapunguzia hasara hiyo, Shirika lake ambalo ni miongoni mwa watekelezaji wa Programu ya AGRI-CONNECT inayolenga kuboresha mnyororo wa thamani wa chai, kahawa na mazao ya bustani liliamua kuwasaidia vifaa vya kisasa.

Alisema mbali na kuwasaidia makreti hayo 800 pia liliwapatia kifaa maalumu cha kuvunia matunda hayo ambacho kitawasaidia kuondokana na njia za kienyeji.

"Programu hii ya AGRI-CONNECT inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na sisi ni miongoni mwa watekelezaji, sasa tumeamua kushirikiana ili wakulima waondokane na hasara ambayo wamekuwa wakiipata," alisema Kalimbya na kuongeza.

"Ukihifadhi matunda kwenye gunia yanaharibika haraka kwa sababu haliingizi hewa ya kutosha, lakini ukihifadhi kwenye vikapu vya mbao yanaharibika kwa sababu mbao ni ngumu," aliongeza.

Vilevile, alisema Shirika hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, wanatarajia kufanya utafiti wa kifaa bora cha kuvunia maparachichi ambacho kitawasaidia wakulima kupunguza upotevu.

Meneja wa UWAMARU AMCOS, Cosmas Kidiga, alisema umoja huo ulianzishwa mwaka 2012, lakini ulisajiliwa mwaka 2018 ambapo umekuwa ukifanya shughuli mbalimbali za kilimo cha maparachichi.

Kidiga alisema kwa sasa umoja huo una wanachama 316 ambao wote ni wakulima wadogo wa maparachichi kutoka katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Alisema wakulima hao wamekuwa wakitumia mbinu za kienyeji kuvuna na kuhifadhi mazao yao kutokana na vifaa vya kisasa kuuzwa kwa bei kubwa ambazo huwa wanashindwa kumudu kuvinunua.

"Tunaishukuru serikali imekuwa ikitusaidia vitu mbalimbali kwenye kilimo cha zao hili, lakini kipekee tunawashukuru HELVETAS wametusaidia sana na tunaahidi kuendelea kushirikiana nao," alisema Kidiga.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya serikali na kuwakabidhi wakulima, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, aliwataka viongozi wa UWAMARU kuvitumia vifaa hivyo kwa kazi iliyokusudiwa ili kuongeza thamani ya zao hilo.

Alisema serikali itahakikisha inalisimamia vizuri zao hilo kutokana na kwamba ni miongoni mwa vyanzo vikubwa vya mapato na kwamba limesaidia kuboresha maisha ya wananchi.



Kazi za ujenzi wa barabara sehemu ya njiapanda ya Nduta – Kibondo Mjini yenye urefu wa KM 25.9 zikiendelea, mkoani Kigoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanakijiji wataka kuacha usafiri wa kutumia mtumbwi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Ikombe, Kata ya Matema wilayani Kyela, wameiomba serikali iwajengee barabara ya kuunganisha kijiji hicho na makao makuu ya kata ili waondokane na usafiri wa kutumia mitumbwi ambayo inahatarisha maisha yao.

Wananchi hao wanadai kuwa wanashindwa kupata huduma muhimu ambazo zinapatikana Matema na hata kuvuka kwenda kupata huduma Kyela Mjini na maeneo mengine ya Mkoa wa Mbeya kwa sababu ya kukosa barabara.

Julius Angumbwike alisema walijaribu kuchimba barabara kwa kutumia jembe la mkono, lakini walikwama kutokana na jiografia ya eneo hilo kuwa na milima na mawe makubwa ambayo yaliwaletea shida.

Alisema barabara hiyo waliichimba pembezoni mwa Ziwa Nyasa na serikali iliwaahidi kuikamilisha barabara hiyo, lakini haijatekeleza.

"Sisi huku biashara yetu kubwa ni vyungu na samaki, lakini wateja wetu wapo Kyela na Mbeya, sasa huwa tunalazimika kusafirisha kwa kutumia mitumbwi kwa sababu magari hayawezi kufika hapa," alisema Angumbwike.

Alisema hata uchumi wao unashindwa kukua kwa sababu ya kukosekana kwa usafiri wa uhakika, hivyo aliiomba serikali iwasaidie ili kukifungua kijiji hicho.

Mbunge wa Kyela, Ally Jumbe, alisema alifanya ziara katika kijiji hicho akiwa ameambatana na maofisa wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa ajili ya kuangalia namna ya kujenga barabara hiyo.

Alisema tatizo la barabara hiyo ni kwamba ina milima yenye miamba mingi ambayo inatakiwa kupasuliwa kwa kulipuliwa na baruti pamoja na kuboresha madaraja na kwamba kuna mkandarasi alitakiwa aijenge barabara hiyo, lakini aliitelekeza.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi wa kijiji hicho kwa sababu kina wananchi wa eneo hilo wanapata huduma muhimu katika maeneo ambayo wanalazimika kupita kwenye maji.

Alisema barabara hiyo na zingine za Kyela Mjini zipo kwenye mipango ya serikali kujengwa, hivyo aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati harakati za ujenzi zikiendelea.

# Agizo la Homera lawasha umeme vijijini

Na Nebart Msokwa, MBEYA

SIKU chache baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kusema haridhishwi na kasi ya usambazaji wa umeme vijijini, Shirika la Umeme nchini (TANESCO) limeanza kuwasha umeme kwenye vijiji ambavyo vimepitiwa na nishati hiyo, lakini wananchi walikuwa hawajaunganishiwa.

Mwishoni mwa wiki maofisa wa TANESCO, waliwasha umeme katika Kijiji cha Mbonile kilichoko katika Kata ya Ulenje ambacho kilikuwa hakijawahi kupata huduma hiyo na wananchi walikuwa wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 10 kwenda kuitafuta vijiji jirani.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mathias Solongo, alisema shirika hilo litaendelea kuwasha nishati hiyo kwenye vijiji ambavyo vipo kwenye miradi ili kuhakikisha wananchi wanafanya shughuli zao kwa amani.

Alisema wanawawashia wananchi wote ambao wameshalipia huduma hiyo, na kwamba wataalamu wanakagua mifumo yote ili kuhakikisha wananchi hawapati madhara kutokana na kutoitumia vizuri nishati hiyo.

Alisema wanawaunganishia wananchi hao umeme kwa gharama ambazo zimeainishwa na serikali, kwamba ambao hawajalipia wanatakiwa waendelee kulipia.

"Tunaendelea na zoezi hili kwenye vijiji mbalimbali na kila mwananchi ambaye ameshalipia ataunganishiwa umeme, gharama ni zile zile zilizoainishwa na serikali kwamba ni Sh. 27,000 maeneo ya vijijini," alisema Mhandisi Solongo.

Wakizungumza baada ya kuunganishiwa nishati hiyo, baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mbonile walisema sasa wataondokana na matumizi ya vibatari pamoja na kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya umeme.

Zainab Richard alisema walikuwa wanatembea umbali mrefu kwenda kupata huduma hiyo katika vijiji vya Simambwe ambako ndiko kwenye huduma hiyo.

Alisema huduma walizokuwa wanazifuata ni kusaga, kuchaji simu pamoja na huduma zingine zinazohitaji huduma hiyo ikiwamo kunyoa nywele.

"Tulikuwa tunalazimika kwenda kuchaji simu zetu Simambwe na kwa wenye uwezo walikuwa wamenunua sola (umeme wa jua), sasa hivi tunawashukuru TANESCO wametuletea umeme hizi huduma tutazipata hapahapa," alisema Zainab.

Naye Peter Mwasapili alisema vijana walikuwa wanashindwa kuanzisha shughuli za ujasiriamali zinazohitaji uwapo wa nishati hiyo.

Alisema wataanzisha shughuli hizo ikiwamo uchomeleaji, vinyozi pamoja na shughuli za viwanda vidogo vidogo kwenye maeneo yao.

Diwani wa Kata ya Ulenje, Mhandisi Boniface Njombe, alisema kuwashwa kwa umeme katika kijiji cha Mbonile italeta chachu ya maendeleo kwa wananchi wake akisema kuwa wakati mwingine walikuwa wanatumia muda mrefu kutembea kwenda kutafuta huduma.

Aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwasogezea huduma wananchi ambapo alisema huduma hiyo itasambaa kwenye taasisi za usimamizi ikiwamo shule za msingi.



# Zanzibar yafurahia ajira, mgawo asilimia 21

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema suala la ajira za Wazanzibari kwenye taasisi za Muungano, mgawo wa asilimia 21 katika taasisi hizo kwa watumishi wa kawaida ukiacha vyombo vya ulinzi na usalama, limepatiwa ufumbuzi.

Hayo yalimesemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua ufumbuzi wa ajira kwa Wazanzibari kwenye taasisi za Muungano.

Waziri huyo alisema suala hilo limepatiwa ufumbuzi na sasa Wazanzibari ruhusa kuomba nafasi za ajira kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Alizitaja juhudi zilizochukuliwa kwa sasa ni pamoja na sekretarieti ya ajira kupatiwa ofisi yake Zanzibar katika eneo la Shangani ambayo kwa sasa wamehamisha shughuli zao hadi Mazizini Unguja.

Alizitaja kazi za sekretarieti hiyo ni pamoja na kusambaza matangazo ya nafasi za ajira za kazi zinapotokea ambazo zinapatikana kupitia tovuti mbalimbali.

Alisema makubaliano hayo yamefikiwa zaidi ya miaka minane, ingawa utekelezaji wake umekuwa ukisuasua kabla ya kuweka masharti na mwongozo wake wa mgao rasmi wa ajira hizo.

Alisema kwa mujibu wa mwongozo wa uwiano wa mgawo wa nafasi hizo, ajira za taasisi za muungano kwa upande wa Tanzania Bara ni asilimia 79.

"Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kwamba suala la mgao wa nafasi za ajira kwa Wazanzibari katika taasisi za muungano tayari tumepatiwa ufumbuzi, kwa upande wa Zanzibar mgao ni asilimia 21 na upande wa Tanzania Bara ni asilimia 79," alisema.

Aidha, alisema ili kukidhi vigezo vya ajira asilimia 21 atakayeomba atalazimika kukidhi vigezo na sifa za nafasi hiyo kwa mujibu wa sheria.




Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman (kushoto), akizungumza na Waziri wa Fedha na Mipango, Jamal Kassim, katika kikao cha Baraza la Wawakishi Chukwa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Kasi ya ajali yaongeza mahitaji ya vyuma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, imekiri kuongezeka kwa kasi ya ajali za barabarani kumesababisha ongezeko la mahitaji ya kununua vyuma kwa ajili ya kutibu viungo vya mwili.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, alipokuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, aliyetaka kujua hatua zinazochukuliwa kukabiliana na ajali za bodaboda na upatikanaji wa vyuma vya viungo.

Mazrui alisema tangu biashara ya bodaboda kuruhusiwa rasmi ajali nyingi zimeripotiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyingine zilioko vijijini.

Alisema ajali nyingi za bodaboda ni zile za kupata matatizo ya viungo vya miguu na mikono au kiuno, na kwamba wanalazimika kutafuta vyuma kwa ajili ya matibabu yake ya awali.

Akifafanua zaidi alisema tayari wamefanya mawasiliano kwa ajili ya kununua vyuma zaidi kwa ajili ya matibabu ya watu wanaopata ajali ili kukidhi mahitaji na mata-

**Mazrui alisema tangu biashara ya bodaboda kuruhusiwa rasmi ajali nyingi zimeripotiwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na hospitali nyingine zilioko vijijini.**

# Dk. Shein aonya ubaguzi uchaguzi ndani CCM

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wanachama wa CCM kutofanya makosa kuchagua viongozi kwa misingi ya ubaguzi katika uchaguzi wa ndani unaotarajia kufanyika mwaka huu.

Alisema wanachama wa CCM hawatakiwi kufanya makosa ya kuchaguana katika uchaguzi huo kwa kubaguana kwa majina na badala yake wanatakiwa kuwachagua viongozi kwa kuzingatia uwezo na sifa.

Kauli hiyo aliitoa wakati akizindua ugawaji wa kadi mpya za CCM za kielektroniki mkoa wa Kaskazini Unguja, huku akieleza kuna haja ya kuhakikisha viongozi hao wanachaguliwa kwa kuzingatia sifa za uwezo wa utendaji na ukereketwa wa CCM kwa kuifahamu chama na misingi yake.

"Tujitahidi sana katika uchaguzi huu kuwa wa waaminifu na wakweli tusiwe wababaishaji hasa kwa kuwatumikia watu sisi tunatasimamia maadili chama hichi kina historia ya misingi ya usawa na haki ya kuwatumikia watu," alisema.

Dk. Shein alisema kuna kazi kubwa mbele ya safari kwa kuwapata viongozi watakaongoza miaka mitano ijayo, na kwamba kuna haja ya kuwachagua watu waliotayari kukitumikia chama.

"Katika jambo hili nafikiria watu hawa tunawajua katika matawi yetu tuna wajua kwa upande wa wilaya tunajuana hata kwenye mkoa hivyo tusiwaweke watu wenye tabia ya kutumatuma hatumii muda kukitumikia CCM," alisema.

Dk. Shein alisema mabadiliko yanayotokea duniani ndiyo imeifanya CCM kuanza kutumia mfumo wa Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na kadi mpya za kielektroniki.

Alisema mfumo wa TEHAMA una mafanikio makubwa zaidi pamoja na umadhubuti wake na kwamba kuna haja ya kuanza kuingia kwenye mfumo huo ikiwamo matumizi ya kadi za kielektroniki.

Kwa mujibu wa Makamu huyo, matumizi ya mfumo wa TEHAMA una faida kubwa na kwamba taarifa za mwanachama zitaweza kubakia hata kama kadi yake ameipoteza.

"Tunatarajia kutoa kadi hizi mpya ili kupata wanachama zaidi na pia ili demokrasia ndani ya chama ikue hivyo chama makini kama CCM lazima kiwe na uhai kila siku kwa kupata wanachama wapya hata hivyo tunapaswa kusimamia misingi ya demokrasia," alisema.

Alisema misingi hiyo ya demokrasia ni pamoja na kuhakikisha inasimamia makusanyo zaidi ya mapato ndani ya chama kuwatumikia wananchi na ufanyaji wa kazi kwa usanifu.

"Wapo wanaofikiria kuwa siku hizi CCM hatujitegemea bado sisi tunategemea na tuendelee kujitegemea mambo mbalimbali tumeweza hivyo kujitegemea ni jukumu letu tangu ASP na TANU," alisema.

Dk. Shein alisema wanachama wa CCM wanapaswa kuunga mkono serikali mbili kutokana na kuwa chama kinaongoza serikali hizo ikiwamo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake, Mjumbe mstaafu wa Kamati Maalum na Makamu wa Pili wa Rais Mstaafu, Balozi Seif Ali Idd, alisema kadi mpya za CCM za kielektroniki ni nzuri kwa kuwa ni rahisi kutunzika.

"Katika uchaguzi huu wanachama mnatakiwa kuhakikisha mnachagua watu wenye uwezo wa kufanya kazi na si kutumikia matumbo yao kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na upendo mkubwa ili kufanikisha dira za CCM," alisema.

Alisema kazi inayofanywa na serikali ya awamu ya nane ni nzuri yenye kuonyesha matumaini makubwa ya kuiona Zanzibar ikipiga hatua.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

FRANK LAZARO SANGA
Anatangaza kupotelewa na Kadi yake ya Pikipiki aina ya BAJAJ BOXER yenye no za usajili MC 327BLK Chassis no MD2A21BZ7DWB15257, Engine no PFZWDB35960 yeyote atakaona au kuokota atoe taarifa Kituo chochote Cha polisi . Taarifa ya Polisi DOD/DOD/RB/79426/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

ABDALLAH AWADHI AHMED
Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba usajili MC 293 CSH yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0714550066
MOR /GAI /RB/63866/2022

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CAUSE NO.27 OF 2018**

**MAUREEN GEORGE MBOWE JILIWA……..1st PLAINTIFF**
**MAUREEN GEORGE MBOWE AS guardian of BARICK BECKAM JILIWA and BARACK GEORGE JILIWA……….2nd PLAINTIFF**
**VERSUS**
**TWIGA BANCORP LTD…………..1st DEFENDANT**
**SAID MUSA MSWAKI………….2nd DEFENDANT**
**NONDO KALOMBOLA t/a N.J PETROLEUM S.P.R.L………………3rd DEFENDANT**
**AMAN ETCHA……….4th DEFENDANT**
**A.K.MAMBA t/a MAMBA AUCTION MART CO.LTD…………5th DEFENDANT**
**SUDI KHAMIS SUDI………………..6th DEFENDANT**

**TO.SAIDI MUSSA MSWAKI**

**WHEREAS** the above named plaintiff has instituted as a suit against you,you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 07th march,2022 at 14:00hrs before Hon.I Arufani,J (room no.1)to answer the said suit and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day before mentioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**Given under my hand and the seal of this court,this 25th day of February,2022**

DEPUTY REGISTRAR

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA KYELA**
**LILILOPO KYELA**
**MAOMBI NA.11/2020**

**KADENA MWAKASYELE…………….MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KELVIN MWAMKINGA……….MJIBU MAOMBI WA 1**
**KAISI KALAMBO(msimamizi wa mirathi ya marehemu ISSA KAISI)……….MJIBU MAOMBI WA 2**
**EMANUEL MWAKIFUNA………MJIBU MAOMBI WA 3**
**LILIAN JONAS GEORGE……..MJIBU MAOMBI WA 4**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA.LILIAN JONAS GOERGE**

Fahamu kwamba,baada ya kutofika shaurini na kutoleta utetezi wako kwa mujibu wa amri na wito wa baraza hili wa tarehe 20/12/2021 kwa kupitia gazeti la nipashe la tarehe 12/01/2022

Shauri la hapo juu limepangwa kuanza kusikilizwa tarehe 02/03/2022 bila uwepo wako mbele ya mheshimiwa B.J Cyril mwenyekiti wa baraza

Amri hii im etolewa kwa mkono wangu na mhuri wa baraza hili leo tarehe 18/01/2022

B.J.Cyril
Mwenyekiti
18/01/2022

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Zaidi ya 500,000 waikimbia Ukraine

- Russia, Ukraine wakutana kutuliza mgogoro
- Wanafunzi Waafrika wadai kukwama mipakani




Baadhi ya wakazi wa Ukraine wakiwa katika makazi maalum ya kujilinda katika eneo la kituo cha michezo mjini Mariupol, nchini humo. Makazi hayo yana uwezo wa kutoa malazi kwa watu 2,000. **PICHA: AP**

IKIWA ni siku ya sita tangu mashambulizi ya vikosi vya Russia dhidi ya Ukraine yaanze, Umoja wa Mataifa (UN), umesema kwamba takribani wakimbizi 500,000 wameyakimbia makazi yao kutoka nchini Ukraine.

Hata hivyo jana, ilikuwa maalumu kwa ajili ya mazungumzo ili kutafuta suluhu kati ya nchi hizo mbili yakifanyika kwenye mpaka wa Ukraine-Belarus, licha ya mashumbulizi kuendelea Ukraine wakati mazungumzo yakiendelea.

Kabla ya mazungumzo hayo yaliyochukua saa kadhaa, ujumbe wa Rais wa Ukraine ulisema inataka kusitishwa mara moja kwa mapigano na kuondolewa kwa vikosi vya Russia, huku Kemlin, Moscow ikitaka yafikiwe makubaliano ambayo yana maslahi ya pande zote mbili.

Mkuu wa Haki za Binadamu UN, Michelle Bachelet, amesema ofisi imethibitisha idadi ya vifo 102 vya raia wakiwamo watoto saba, huku 304 wakijeruhiwa tangu Alhamisi wiki iliyopita, mashambulizi yalipoanza.

Aidha, taarifa ya Wizara ya Afya Ukraine, inasema hadi sasa vifo ni vya watu 352, wakiwamo watoto 14.

"Wengi wa raia hawa wameuawa kwa milipuko ya mabomu na roketi kwenye mashamblizi ya angani," Bacheletb akiwa mjini Geneva, jana.

Kamishna Mkuu wa Wakimbizi UN, Filippo Grandi kwenye ukurasa wake wa Tweeter, anasema watu 281,000 wameingia nchi ya Poland, 84,500 wameingia Hungary, huku 36,400 wakiingia Moldova. Kadhalika watu 32,500 wakiingia nchini Romania pia 30,000 wakikadiriwa kuingia Slovakia, kwa mujibu wa Msemaji wa UNHCR.

### WANAFUNZI WAAFRIKA

Mwandishi wa habari wa Ajazeera, anasema wanafunzi kadhaa kutoka nchi za Afrika Magharibi ikiwamo Nigeria, Ghana wamekwama mjini Dnipro, Ukraine wa takribani saa 48 kutokana na kukosa usafiri kutoka eneo hilo.

Baadhi ya wanafunzi hao, ikiwamo kutoka India, wamesambaza picha za video mtandaoni kuelezea vikwazo wanavyokumbana navyo wakidai wanabaguliwa kutopewa kipaumbele cha kuvuka mipaka na kuondoka Ukraine, licha ya kuwa na pasi za kusafiria.

Balozi wa Nigeria nchini Romania, Safiya Nuhu, aliiambia BBC, takriban Wanigeria 200 wengi wao wakiwa wanafunzi, wamewasili katika mji mkuu wa Bucharest kutoka Ukraine na

Wizara ya Mambo ya Nje Nigeria, ilikuwa imewashauri Wanigeria wanaoondoka Ukraine kujaribu kuvuka mpaka wa Hungary na Romania, kutokana na mgogoro ulioko kwenye mpaka wa Poland.

Pia mwanafunzi Salum Msabaha, anayesoma Chuo cha Suni kilichoko Mashariki mwa Ukraine, anasema wanafunzi wameambiwa wakae ndani huku wakiendelea kusikia milio ya risasi maeneo ya jirani na makazi yao.

"Kuna muda tunatoka kwenda kutafuta chakula kwa muda mchache, tunakwenda supermarket za karibu huwa wazi muda mfupi. Nje kidogo na mji tuliopo si salama sana kwa sababu kuna milio ya risasi, kuna muda umeme ulizimwa eneo lote hili, wengi wetu tuna wasiwasi," anasema Msabaha akizungumza na DW.

**Kuongezeka kwa operesheni za kijeshi ya Russia nchini Ukraine kunasababisha kuongezeka kwa ukiukwaji wa haki za binadamu.**

Mwanafunzi mwingine wa chuo kikuu Ruqqaya, kutoka Nigeria, alikuwa akisomea udaktari huko Kharkiv Mashariki mwa Ukraine, wakati mji huo uliposhambuliwa. Alitembea kwa saa 11 usiku kucha, kabla ya kufika kwenye kivuko cha Medyka na Poland.

"Nilipokuja hapa kulikuwa na watu weusi wamelala barabarani," aliiambia BBC.

Anasema aliambiwa na walinzi waliokuwa na silaha kusubiri raia wa Ukraine kupitishwa kwanza.

Anasema alitazama mabasi ya watu, ambao aliwataja kuwa wazungu, waliruhusiwa kupita mpakani huku Waafrika wachache tu wakichaguliwa kutoka kwenye foleni. Baada ya kungoja kwa saa nyingi, hatimaye aliruhusiwa kuvuka na kuelekea Warsaw kwa ndege kurudi Nigeria.

Asya, mwanafunzi wa utabibu kutoka Somalia, anayesoma Kyiv, alikumbana na tukio kama hilo. Hatimaye alipofika Poland, aliambiwa: "Malazi katika hoteli ni ya Waukraine pekee".

Kikosi cha mpakani cha Poland kiliiambia BBC kwamba kila mtu anayekimbia mzozo nchini Ukraine anakaribishwa nchini Poland, bila kujali utaifa.

### BARAZA KUU UN

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, limekutana juzi kwa dharura mjini New York, Marekani kupiga kura ya azimio la kuitisha kikao maalum cha nadra cha wajumbe wote 193 wa baraza hilo, kuhusu uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres kwenye kikao hicho, alisema: Kuongezeka kwa operesheni za kijeshi Russia nchini Ukraine, kunasababisha kuongezeka kwa ukiukaji wa haki za binadamu."

"Kuongezeka kwa operesheni za kijeshi ya Russia nchini Ukraine kunasababisha kuongezeka kwa ukiukwaji wa haki za binadamu," anasema Guterres.

Baraza la Usalama lenye wanachama 15 kwa utaratibu huo hakuna hata mmoja kati ya wajumbe watano wa kudumu wa baraza hilo, ambao ni Russia, China, Ufaransa, Uingereza na Marekani, anayeweza kutumia kura yake ya turufu.

Hatua hiyo inahitaji kura tisa za ndio ili kupitishwa ili kuitisha kikao cha baraza hilo.

Azimio la kuitishwa kikao ilipitishwa baada ya wajumbe 11 kupiga kura ya ndio. Mjumbe mmoja ambaye ni Russia, ilipiga kura ya hapana na wajumbe watatu ambao ni China, India na Umoja wa Falme za Kiarabu Emirate (UAE) wakijizuia kupiga kura.

Muswada wa azimio hilo, umepewa namba 2623-2022. Kupitishwa kwa muswada huo wa azimio kutafanya baraza hilo, kukutaka kwenye kikao hicho maalum cha dharura ikiwa ni awamu ya 11 tangu mwaka 1950.

Azimio hilo 377A lilipitishwa tarehe 3 Novemba 1950 baada ya mjadala wa siku 14 za mjadala wa Baraza kuu na kupigiwa kura na wajumbe 59 wa wakati huo ambapo lilipita kwa kura 52 za ndio, 5 za hapana na mjumbe mmoja hakupiga kura.

Kwa mujibu wa azimio hilo kikao maalumu kinapaswa kufanyika ndani ya saa 24 tangu Baraza la Usalama kupitisha muswada wa azimio wa kuomba kikao hicho.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale, kwa msaada wa vyanzo mbalimbali vya habari.**

# AZAM, COASTAL VITANI LIGI KUU ZIKITOKA KUJERUHIWA

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara inaendelea leo katika Uwanja wa Azam Complex, kwa wenyeji Azam FC kuikaribisha Coastal Union ya Tanga.

Azam FC itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi yao ya kufunga mzunguko wa kwanza baada ya kushindiliwa mabao 2-0 dhidi ya Biashara United kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Kwa upande wa Coastal Union nao wanashuka dimbani wakitoka kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Geita Gold FC ambao walikuwa nyumbani kwenye mechi hiyo.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti jana makocha wa wasaidizi wa timu hizo, kila mmoja alieleza dhamira yao ya kuibuka na alama tatu kwenye mechi hiyo.

Kwa upande wa Azam FC, Kocha Msaidizi, John Yona, alisema wanahitaji kupata pointi tatu ili kuzikimbia Mbeya City, Namungo FC ambazo wana pointi sawa (24) katika msimamo wa ligi hiyo.

"Coastal Union ni timu nzuri tunawaheshimu, tunashuka dimbani kwa nidhamu kubwa ya kutafuta pointi muhimu katika mchezo huu," alisema John.

Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, alisema wamejiandaa vizuri kusaka pointi katika mchezo huo mbele ya wenyeji wao, Azam FC.

Alisema anatambua mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu wote wanahitaji kupata pointi muhimu ili kujikita katika nafasi nzuri katika msimamo.

"Mechi zimekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imetoka kupoteza, tumefanyia kazi mapungufu yetu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita na kuhakikisha tunapata pointi dhidi ya Azam FC," alisema Lazaro.

Azam ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 24, wakati Coastal Union ikishika nafasi ya tatu kutoka mkiani na pointi zake 17 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 15.

## Prisons, Dodoma Jiji vinara kujifunga

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za Tanzania Prisons na Dodoma Jiji, zimeweka rekodi ya kuongoza kwa wachezaji wake kujifunga wenyewe kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Kati ya mabao 11 ya kujifunga yaliyopatikana hadi kumalizika kwa mzunguko huo, sita yanazihusu timu hizo mbili, kila moja ikijifunga mara tatu.

Prisons ambayo inashika mkia mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, wachezaji wake wameweka mpira ndani ya nyavu zao wenyewe mara tatu kati ya mabao 21 iliyoruhusu hadi mzunguko wa kwanza unamalizika. Wachezaji hao ni Adil Buha, Michael Mhesa na Vedatus Steven.

Kwa upande wa Dodoma Jiji iliyoko nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi hiyo, wamejifunga mara tatu kati ya mabao 19 waliyoruhusu hadi sasa, wachezaji waliocheka na nyavu zao ni Augustine Nsata, Hussein Masalanga na Justin Bilal.

Timu ya Polisi Tanzania ndiyo inayofuatia kwa wachezaji wake kujifunga, wakiwa wamefanya hivyo mara mbili. Wachezaji wa Polisi Tanzania waliojifunga wenyewe ni Detius Peter na Yahya Mbegu.

Wachezaji wengine ambao wamejifunga mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza ni Abdumalik Zacharia wa Namungo, Kelvin Nashon wa Geita Gold, na Michael Masinda wa Ruvu Shooting.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Mohamed Mussa, akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa Kongamano la Mpira wa Miguu Tanzania maarufu Tanzania Football Summit (TFS), uliofanyika visiwani Zanzibar juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Kongamano la Soka 2022 lazinduliwa Z'bar*

**Na Mwandishi Wetu**

KONGAMANO la Mpira wa Miguu Tanzania maarufu kama Tanzania Football Summit (TFS) kwa mwaka 2022, limezinduliwa rasmi visiwani Zanzibar juzi lengo likiwa ni kuboresha michezo na kutumia watu maarufu duniani ili kuitangaza nchi kimataifa.

Akizindua kongamano hilo ambalo linatarajiwa kufanyika Juni 25 hadi 26, mwaka huu visiwani Zanzibar, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Lela Mohamed Mussa, alisema lengo la serikali zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuboresha michezo.

"Kufanyika kwa kongamano hili Juni mwaka huu hapa Zanzibar, tunatarajia kutumia watu mbalimbali maarufu duniani ambao watakuwa chachu ya kutangaza utalii wa kimichezo nchini. Huu ni wakati muafaka wa kutangaza vyakula vyetu vya hapa, nataka wakati wa kongamano wageni wetu wale vyakula vyetu vinavyotokana na bahari, wale samaki wa hapa kwetu," alisema Waziri Lela.

Lela aliongeza kuwa kongamano hilo la TFS, limekuja muda muafaka likiongozwa na kaulimbiu ya mwaka huu inayosema "Maendeleo ya Mpira wa Miguu kwa Uchumi wa Buluu" kuwa ni hatua ya kuunga mkono sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya Awamu ya Nane chini ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi inayolenga katika matumizi endelevu ya raslimali za bahari katika kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Akipokea taarifa ya kongamano la mwaka 2021, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Tanzania Bara, Saidi Yakubu Yakubu, alisema aliahidi kuyafanyia kazi maazimio ya mwaka jana na kuwapongeza waandaaji wa kongamano kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Mwinyi inayojali michezo katika kujenga uchumi.

Pia aliipongeza kamati maalum inayoandaa kongamano la mwaka huu ambapo tayari mada zake zimeandaliwa kwa wakati.

Yakubu alisema mchezo wa soka una fursa kubwa katika ujenzi wa uchumi wa taifa na kwamba unamchango mkubwa kwenye mapato ya serikali kupitia ligi mbalimbali zinazoendeshwa nchini.

Aliongeza kuwa utalii wa kimichezo umekuwa kiungo muhimu katika nchi ambayo inalenga kuendesha michezo kisayansi na kusema Zanzibar ina maeneo mazuri ya kuwekeza kwenye sekta ya michezo zikiwamo fukwe na bahari ambazo ni vivutio vya watalii.

Kwa upande wake Katibu wa Kamati ya Maalum ya Maandalizi ya kongamano hilo, ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Afrisoccer inayojishughulisha na shunghuli za michezo, Peter Simon, alisema walengwa wakuu wa kongamano hilo ni wadau mbalimbali wa mpira ikiwamo serikali, wasimamizi wa mpira wa miguu ambao ni Shirikisho la Soka, klabu, makocha, wachezaji wa zamani, wawekezaji, kampuni binafsi, mawakala, waandishi wa habari na wapenzi na mashabiki wa mpira wa miguu.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI ATAKIWA MAREKANI

KLABU ya Inter Miami itapambana kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi kama nyota huyo mwenye miaka 34 ataamua kuondoka Paris St-Germain, amesema mmiliki mwenza wa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Marekani, David Bekham. (***Goal***)

### LEWANDOWSKI HAKIELEWEKI

MKATABA wa mshambuliaji wa Poland, Robert Lewandowski pale Bayern Munich unamalizika mwaka 2023, wakati mkongwe huyo mwenye miaka 33 akitaka mkataba mpya ili kusalia katika klabu hiyo ya Ujerumani, hakuna mazungumzo yaliyofanyika mpaka sasa. (***Fabrizio Romano***).

### HAALAND AIKATAA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland hajakubali kujiunga na Real Madrid katika dirisha lijalo la majira ya joto, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake na mshambuliaji wa zamani wa Middlesbrough, Jan Aage Fjortoft mwenye umri wa miaka 21. (***Mundo Deportivo***)

### KESSIE KUTUA BARCA

BARCELONA wanakaribia kumsajili kiungo wa Ivory Coast, Franck Kessie kwa uhamisho huru wakati mkataba wa nyota huyo wa AC Milan mwenye umri wa miaka 25 utakapomalizika. (***Sport***)

### BOTMAN HUYOOO MILAN

KLABU ya Newcastle United ilishindwa kumsajili mlinzi wa Uholanzi, Sven Botman Januari, na kinda huyo mwenye miaka 22 ambaye anahusishwa pia na Tottenham, anatarajia kujiunga na AC Milan katika majira yajayo ya joto. (***Todofichajes***)

### CHRISTENSEN MAMBO MAGUMU

ANDREAS Christensen ameelezea suala lake ndani ya Chelsea ni "gumu", huku mkataba wa mlinzi huyo wa Denmark mwenye miaka 25 ukielekea ukingoni mwisho mwa msimu. (***90 Min***)

### INACIO KUSAINI TENA SPORTING

MLINZI wa Sporting Lisbon, Goncalo Inacio amekubali kusaini mkataba mpya wa kusalia klabuni hapo. Kinda huyo mwenye umri wa miaka 20 alikuwa akiwaniwa na Newcastle United katika dirisha la Januari. (***Fabrizio Romano***)

### ATALANTA KWA DIMITRIS

KLABU za Real Sociedad na Atalanta zinamwania kwa mkopo mlinzi wa kushoto, Dimitris Giannoulis kutoka Norwich City. (***Norfolk Live***)

### SIMEONE ATAKIWA UNITED

KIUNGO wa zamani wa Manchester United, Roy Keane ameiambia klabu hiyo kumpa mikoba ya ukocha, kocha wa sasa wa Atletico Madrid, Diego Simeone. (***Goal***)

### MAX KUITWA ENGLAND

MLINZI wa Wolves, Max Kilman yuko katika kinyang'anyiro cha kuitwa na kocha wa England, Gareth Southgate kwa mechi mbili za kirafiki Machi. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# XAVI AMPELEKA PEDRI ANGA ZA INIESTA BARCA

**Jinsi anavyoelewa mchezo, inapendeza kumtazama akicheza, ananikumbusha mengi kuhusu...**

**BARCELONA,** HISPANIA

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi amemlinganisha Pedri na gwiji wa klabu hiyo, Andreas Iniesta, huku akisifu uchezaji wa Ousmane Dembele dhidi ya Athletic Bilbao.

Bao la nne la Pierre-Emerick Aubameyang katika mechi zake mbili zilizopita za LaLiga liliifanya timu hiyo ya Katalunya kuidhibiti Athletic Jumapili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0.

Dembele aliyetokea benchi ambaye mustakabali wake bado uko shakani baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya kuongezwa mkataba mpya, alifunga bao moja na kusaidia mengine mawili, yaliyofungwa na Luuk de Jong na Memphis Depay.

Dembele amekuwa mchezaji wa kwanza wa akiba wa Barca kuhusika katika mabao matatu katika mchezo mmoja wa LaLiga katika karne ya 21.

Baada ya kurejea kwenye nafasi nne za juu za LaLiga kwa ushindi wa 4-0, Xavi alitoa sifa za pekee kwa Pedri na Dembele.

Xavi alisema: "Jinsi (Pedri) anavyoelewa mchezo, inapendeza kumtazama akicheza. Ananikumbusha mengi kuhusu Andres Iniesta, sijaona vipaji vingi kama hivyo.

"Naona matukio mengi kwa Dembele, tumemwona Dembele ambaye tunamtaka na tunajua ana uwezo wa kufanya."

Alipoulizwa kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa atasalia katika klabu hiyo, Xavi aliongeza: "Hilo si jambo langu tena, nimekuwa nikisema kwamba ana kipaji cha aina yake."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 985

MECHI KALI
BURNLEY
VERSUS
LEICESTER
1 | 2.91
X | 3.31
2 | 2.42

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TUCHEL AKATAA KUMLAUMU KEPA



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, alikataa kumlaumu golikipa Kepa Arrizabalaga kwa timu yake kupoteza fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Liverpool, akisisitiza kuwa “hajutii” baada ya kushindwa.


Baada ya timu zote kukataliwa mabao katika sare ya bila kufungana, mikwaju 21 ya kwanza ya penalti ilifanikiwa, kabla ya Kepa kukosa penalti yake na kuipa Liverpool kombe la kwanza la nyumbani tangu mwaka 2012.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alichukua nafasi ya Edouard Mendy akitokea benchi muda wa ziada kwa lengo la kuisaidia Chelsea kushinda kwa mikwaju ya penalti, baada ya kufanya vema katika hali kama hiyo wakati wa ushindi wa Super Cup dhidi ya Villarreal Agosti mwaka jana.

Tuchel alisema: “Ninajisikia vibaya kwake, lakini (hakuna) lawama. Ikiwa unataka kumlaumu mtu, nilaumu mimi. Ninachukua maamuzi na sichukui kuwa shujaa.

“Tulichukua uamuzi kama tulivyofanya mara ya mwisho (katika Super Cup) kwenye mikwaju ya penalti.

“Kila mtu anajua jinsi alivyo mzuri. Kwa bahati mbaya, hakuweza kuokoa, ambazo zilipigwa kwa ustadi.”



# Ibrahimovic: Sitaondoka Milan hadi nishinde kitu

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic ameapa kuwa hataachana na maisha yake ya soka hadi “nikishinda kitu na timu hii ya AC Milan”.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden alishereheheka mafanikio ya Scudetto mwaka 2011 akiwa na Milan na kutwaa Supercoppa Italia msimu uliofuata, lakini kikosi hicho cha kocha Stefano Pioli bado hakijabeba kombe lolote tangu mshambuliaji huyo arejee mwaka 2019.

Rossoneri hao wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Kikosi cha Pioli pia bado kiko katika kinyang’anyiro cha kuwania Coppa Italia huku wakimenyana na majirani zao Inter Milan katika mechi ya nusu fainali ya mikondo miwili, mkondo wa kwanza utakaofanyika leo Jumanne.

Ibrahimovic, ambaye amekuwa nje ya uwanja kutokana na jeraha la kifundo cha mguu alilopata dhidi ya Juventus Januari 23, anasisitiza kuwa hatastaafu hadi ashinde kitu akiwa na kikosi cha sasa cha Milan.

Alisema: “Mustakabali wangu ni soka, dunia yangu ni soka.

“Nimesikitishwa
kushindwa kucheza k
sasa, hii inaniuma sa
hasa timu inapofanya
zuri.

“Nataka kuwapo na k
saidia timu. Tumefan
mambo makubwa tan
nilipowasili, na sasa tu
kosa kipengele kimoja
kombe.

“Tunapambana kufa
kisha hili, sitaacha ha
nishinde kitu na timu
ya Milan.”

Ibrahimovic ali
geza mkataba wa mwa
mmoja katika klabu
Milan Aprili mwaka ja
ili kumweka katika kla
hiyo hadi mwishoni m
msimu.

HABARI MICHEZO

,669,400

# MAYELE ATOA MKAKATI WA UBINGWA, KIATU LIGI KUU

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa Yanga, Fiston Mayele, amesema ataendelea kutupia mabao kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, lego ikiwa ni kuipa ubingwa timu hiyo ambayo haijaugusa kwa misimu minne.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mayele ambaye alifunga mabao mawili juzi usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Kagera Sugar, alisema ataendelea kufunga kwa sababu lengo lao msimu huu kama timu ni kuchukua ubingwa wa Tanzania Bara na kama ikiwezekana na yeye kuwa mfungaji bora.**

"Kagera Sugar ni timu nzuri, walikuwa wanataka pointi tatu kwetu, lakini sisi Mungu ametusaidia tumeshinda mechi. Malengo yetu msimu huu ni kuchukua ubingwa na ndiyo maana unaona nimekuwa nikijitahidi kufunga mabao kufanikisha hilo nikishirikiana na wenzangu, na hii ilikuwa ni mechi ya kwanza ya mzunguko wa pili, tumebakisha mechi 14, tutaendelea kupambana," alisema Mayele ambaye timu yake ya Yanga iliondoka na ushindi wa mabao 3-0.

Kuhusu ufungaji bora alisema kwa sasa akili yake ni kuipa Yanga ubingwa, lakini kwa sababu anaendelea kufunga mabao, ataendelea pia kufunga ili kuona kama kuna uwezekano wa kuchukua Kiatu cha Dhahabu.

"Nimefunga na nitaendelea kufunga mabao, kwa hiyo naweza kuwa mfungaji bora kama nitawazidi wenzangu," alisema.

Mayele aliwataka wapenzi na mashabiki wa Yanga kujitokeza kwa wingi pale timu hiyo inapokuwa inacheza kwa ajili ya kuwapa sapoti wachezaji ili kuwapa hamasa ya kupambana.

"Sisi tukiona mashabiki wamejaa uwanjani, tunaongeza juhudi kwa sababu tunataka wasiondoke wanyonge, wafurahi," alisema. Kwa sasa straika huyo ana mabao tisa, moja nyuma ya kinara wa mabao kwa sasa, Reliants Lusajo wa Namungo FC mwenye mabao 10.



# Kaseja atoa siri ya kudumu



Na Adam Fungamwago

KIPA mkongwe nchini Juma Kaseja, amesema ameendelea kudumu kwenye soka kwa zaidi ya miaka 20 sasa kutokana na kufuata miiko ya mchezo huo, pamoja na kusikiliza ushauri kutoka kwa watu wote wakubwa kwa wadogo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Kaseja, kipa wa zamani wa klabu za Moro United, Mtibwa Sugar, Simba, Mbeya City, na sasa akiidakia timu ya KMC, amesema kwenye soka kuna vitu wanakatazwa wasifanye, lakini kama mchezaji atakiuka miiko na misingi hata kama kwa kujificha, basi hatodumu kwenye soka kwa muda mrefu kama yeye, awe kipa au mchezaji wa ndani.

"Mpira una makatazo yake na una makubaliano yake, kuna vitu mnakatazwa usifanye na hutakiwi kuvifanya, pia kuna vitu unatakiwa uvifanye kama vile ule vizuri, ulale mapema, na ufanye mazoezi kwa jitihada na unatakiwa kumsikiliza kila mtu anayekwambia, awe mkubwa awe mdogo. Kama una malengo itabidi ufuate yote yanayotakiwa kwa sababu hii ndiyo kazi yako, inayofanya iingize kipato cha kuendesha maisha yako wewe na familia yako," alisema kipa huyo ambaye mara kwa mara huitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars.

Kaseja alisema kuwa yeye amekuwa muumini wa kufuata miiko hiyo, na siyo kama amedumu kwa muda mrefu kwenye soka tu, lakini hana historia ya kukumbwa na majeraha makubwa au ya kudumu.

"Hii ndiyo sababu kubwa nafuata vyote hivyo, nidhamu na ndiyo maana inanifanya pia nisiwe na majeraha na nafanya sana mazoezi kwa bidii na kwa kujitolea, hadi leo niko fiti na naendelea na soka," alisema.

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/03/22 | 18:00 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.09 | 3.34 |
| 02. 05/03/22 | 18:00 | Newcastle vs Brighton | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 03. 05/03/22 | 18:00 | Aston Villa vs Southampton | 2.30 | 3.36 | 3.06 |
| 04. 05/03/22 | 18:00 | Norwich City vs Brentford | 2.95 | 3.10 | 2.50 |
| 05. 05/03/22 | 20:00 | Roma vs Atalanta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 06. 06/03/22 | 14:30 | Genoa vs Empoli | 2.61 | 3.26 | 2.71 |
| 07. 06/03/22 | 16:00 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 3.31 | 3.06 | 2.32 |
| 08. 06/03/22 | 17:00 | Reims vs Strasbourg | 3.48 | 2.78 | 2.39 |
| 09. 06/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Troyes | 2.29 | 3.48 | 2.93 |
| 10. 06/03/22 | 17:00 | Bologna vs Torino | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 11. 06/03/22 | 19:00 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 12. 06/03/22 | 19:00 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.38 | 3.21 | 2.91 |
| 13. 06/03/22 | 19:30 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.70 | 3.40 | 2.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 01/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 3380 | Peterborough United Reserve vs Crewe U23 | 1.41 | 4.71 | 5.57 |
| 16:00 | 3487 | Sheffield United U23 vs Hull City U23 | 1.33 | 5.03 | 6.58 |
| 16:00 | 3766 | Cardiff City U23 vs Bristol City U23 | 1.97 | 3.67 | 3.13 |
| 16:00 | 4415 | Coventry U23 vs Barnsley U23 | 1.43 | 4.64 | 5.41 |
| 16:00 | 4744 | Colchester U23 vs Charlton U23 | 3.03 | 3.76 | 1.98 |
| 16:00 | 4913 | QPR U23 vs Millwall U23 | 1.96 | 3.71 | 3.13 |
| 18:30 | 3340 | Dinamo Bucuresti vs Sepsi Osk | 3.83 | 3.39 | 1.91 |
| 19:00 | 1645 | Levadia Tallinn vs Tallinna Kalev | 1.01 | 16.40 | 43.42 |
| 19:15 | 5374 | Kazincbaricika SC vs Paksi FC | 6.93 | 5.39 | 1.30 |
| 20:00 | 1863 | Olimpia Grudziadz vs Wisla Krakow | 8.68 | 5.02 | 1.27 |
| 20:00 | 2987 | Dinamo Moscow vs Nizhny Novgorod | 1.32 | 4.52 | 8.28 |
| 20:30 | 1501 | Brescia vs Perugia | 2.17 | 3.09 | 3.38 |
| 20:30 | 4521 | Ternana vs Pordenone | 1.67 | 3.49 | 5.11 |
| 20:30 | 5258 | Benevento vs Cremonese | 2.22 | 3.03 | 3.33 |
| 20:55 | 2205 | U Craiova SA vs Rapid Bucuresti | 2.40 | 2.99 | 3.04 |
| 21:00 | 1718 | Parnu JK Vaprus vs Paide Linnameeskond | 20.33 | 8.32 | 1.07 |
| 21:00 | 5577 | 1860 Munich vs Kaiserslautern | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 21:30 | 1620 | FC Schaffhausen vs FC Stade LS Ouchy | 2.14 | 3.37 | 2.98 |
| 21:30 | 3804 | FC Thun vs Neuchatel Xamax | 1.93 | 3.57 | 3.32 |
| 22:00 | 2049 | Creteil vs Sete 34 FC | 2.25 | 3.07 | 3.17 |
| 22:00 | 2878 | Villefranche Sur Saone vs Boulogne | 2.05 | 2.98 | 3.81 |
| 22:00 | 4282 | Budapest Honved vs Ferencvaros TC | 3.46 | 3.56 | 1.89 |
| 22:00 | 4678 | Emmen vs Helmond Sport | 1.20 | 6.21 | 10.68 |
| 22:15 | 4876 | Peterborough vs Manchester City | 18.90 | 7.72 | 1.12 |
| 22:30 | 1466 | Arbroath vs Partick Thisle | 2.33 | 3.31 | 2.82 |
| 22:30 | 3072 | Crystal Palace vs Stoke City | 1.69 | 3.70 | 4.73 |
| 22:30 | 3161 | Servette Geneva vs BSC Young Boys | 3.36 | 3.46 | 2.05 |
| 22:30 | 5967 | Alessandria vs Como | 2.30 | 3.03 | 3.18 |
| 22:45 | 1514 | Wigan vs Fleetwood Town | 1.48 | 4.23 | 5.90 |
| 22:45 | 1632 | Carlisle vs Rochdale | 3.00 | 3.20 | 2.30 |
| 22:45 | 1947 | Arka Gdynia vs Rakow Czestochowa | 4.23 | 3.70 | 1.68 |
| 22:45 | 2405 | Bristol Rovers vs Barrow | 2.03 | 3.29 | 3.54 |
| 22:45 | 2685 | Northampton vs Walsall | 1.95 | 3.28 | 3.82 |
| 22:45 | 2705 | Sheffield Wed vs Burton | 1.68 | 3.70 | 4.63 |
| 22:45 | 2752 | Cardiff vs Derby | 2.01 | 3.15 | 3.79 |
| 22:45 | 2957 | Harrogate vs Port Vale | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 22:45 | 3284 | Newport vs Forest Green | 2.56 | 3.20 | 2.66 |
| 22:45 | 3353 | Burnley vs Leicester | 2.91 | 3.31 | 2.42 |
| 22:45 | 3355 | Wycombe vs Cambridge Utd | 1.80 | 3.60 | 4.04 |
| 22:45 | 3612 | Chesterfield vs Notts County | 2.33 | 3.26 | 2.87 |
| 22:45 | 3832 | Shrewsbury vs Rotherham | 4.71 | 3.58 | 1.70 |
| 22:45 | 3987 | Colchester vs Leyton Orient | 2.65 | 3.09 | 2.65 |
| 22:45 | 4064 | Queens Park vs Peterhead | 1.66 | 3.76 | 4.59 |
| 22:45 | 4127 | Union Berlin vs St. Pauli | 1.83 | 3.64 | 4.19 |
| 22:45 | 4621 | Crawley Town vs Oldham | 2.08 | 3.34 | 3.34 |
| 22:45 | 4864 | Portsmouth vs Oxford Utd | 2.40 | 3.28 | 2.79 |
| 22:45 | 5133 | Coleraine FC vs Larne | 2.31 | 3.52 | 2.60 |
| 22:55 | 3786 | Middlesbrough vs Tottenham | 4.52 | 3.78 | 1.70 |
| 23:00 | 1438 | Nice vs FC Versailles 78 | 1.20 | 6.10 | 12.79 |
| 23:00 | 4671 | AC Milan vs Inter | 2.85 | 3.44 | 2.30 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Machi 1, 2022

Nipashe




Pedri apelekwa anga za Iniesta UKURASA 21

# Pablo: Sababu kipigo Simba Morocco ni hii

●●● Amsifu pia aliyemtungua Manula akiwapongeza wachezaji wake, waingia mawindoni Ligi Kuu, huku...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba Pablo Franco (pichani) amesema hali ya hewa, kukosekana kwa baadhi ya wachezaji muhimu, pamoja na makosa binafsi ya wachezaji ndiyo yaliyosababisha kupoteza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF) hatua ya makundi kwa kufungwa mabao 2-0 juzi usiku kwenye Uwanja wa Municipal de Berkane dhidi ya RS Berkane.

**Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Pablo alisema wachezaji wake walijitahidi mno kupambana na wenyeji, lakini hali ya hewa iliwaathiri, pia timu yake inapitia kipindi kigumu kwa kuwakosa wachezaji wengi muhimu.**

"Hali ya hewa haikuwa nzuri, nimewakosa asilimia 41 ya wachezaji wangu. Goli la kwanza huwezi kumlaumu golikipa Aishi Manula, badala yake kumsifu mpigaji, bao la pili lilitokana na uzembe wa mabeki, tukafungwa bao rahisi, lakini mabeki wangu walicheza baadhi ya faulo ambazo hazikuwa na umuhimu wowote, huku tukifungwa mabao yote kwa njia ya faulo," alisema kocha huyo.

Alisema kipindi cha pili walijitahidi kupunguza makosa na kuwa makini, kiasi cha kufanya mashambulizi kadhaa, na kugongesha mwamba.

Hata hivyo, alisema amefurahi kuona wachezaji wake wamecheza vizuri, huku ikiwa ni timu pekee ambayo mpaka sasa imepata sare ugenini.

"Sisi ndiyo timu pekee ambayo tumetoa sare kwenye kundi letu, kwa hiyo inatupa matumaini ya kusonga mbele," alisema.

Simba iliwakosa wachezaji Jonas Mkude, Paschal Wawa, ambao walikuwa majeruhi, huku Thadeo Lwanga naye akiwa hajapona vizuri, lakini wachezaji Mzamiru Yassin na Rally Bwalya wakiwa hawajasafiri na kikosi hicho.

Winga wa zamani wa timu hiyo, Thomas Kipese amesema tatizo la Simba la muda mrefu ni kufungwa mabao ya kona na faulo.

"Kwa muda mrefu Simba wanafungwa sana mabao ya kona na faulo, mwalimu anatakiwa alisimamie hilo, pia kwa sasa ina matatizo kwenye upande wa ushambuliaji, na pia bado simkubali, Saido Kanoute kwenye kupiga pasi za mwisho, ana matatizo sana," alisema.



Kipese ambaye aliichezea Yanga, kabla ya kujiunga na Simba katikati ya miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, alisema matokeo waliyoyapata Simba ugenini aliyatarajia na si mabaya sana.

"Nilitegemea kwenye mechi mbili anazokwenda kucheza ugenini anaweza kupata pointi moja na kweli, kilichobakia ni kujipanga kushinda mechi mbili za nyumbani," alisema Kipese.

Straika hatari wa zamani wa timu hiyo, Dua Said, yeye amelia na upangaji wa kikosi, akisema kuwa wachezaji kama Bernard Morrison walitakiwa waanze na si kusubiri kipindi cha pili.

"Kuna wachezaji ni wazuri kwenye mechi kubwa. Mchezaji kama Morrison alitakiwa aanze mechi ile na sidhani kama wangeshambulia vile, matokeo yake wameruhusu mabao mawili ambayo yamewanyong'onyeza wachezaji," alisema straika huyo.

Kwa matokeo hayo, Simba imeshuka hadi nafasi ya pili kwenye Kundi D, kwa kuwa na pointi 4, sawa na US Gendamarie ya Niger, RS Berkane ikiwa kileleni kwa pointi sita.

**Wakati huo huo**, kikosi cha Simba kilitarajiwa kurejea jana na Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu alisema baada ya kurejea wachezaji wataelekea moja kwa moja kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Biashara United na Dodoma Jiji kabla ya Machi 13, mwaka huu, kuikaribisha RS Berkane katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya marudiano.

HAKUNA NJIA...



Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akikabiliana na mchezaji wa RS Berkane kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Municipal de Berkane nchini Morocco na wenyeji kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: SIMBA**

# Nabi awachambua Mayele, Ntibazonkiza

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Yanga, Nasreddine Nabi, amefunguka kwa kueleza namna anavyofurahishwa na muunganiko mzuri kati ya Fiston Mayele na Said Ntibazonkiza, ambao umekuwa chachu ya timu hiyo kufanya vizuri.

Nabi alitoa kauli hiyo juzi baada ya mchezo kati Yanga na Kagera Sugar kumalizika kwa kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"'Combination' (muunganiko) ya Mayele na Ntibazonkiza ni nzuri inasaidia kwa kiasi kikubwa timu yangu kuzidi kufanya vizuri katika michezo yake ya Ligi Kuu ya NBC," alisema Nabi.

Alisema kwenye mchezo huo kipindi cha kwanza mchezaji wake, Denis Nkane alionyesha mapungufu kidogo kutokana na kuwa bado hajazoeana na wachezaji wenzake na kwamba siku zinavyozidi kwenda atakuwa vizuri.

Kocha huyo alisema anafurahi kuona wachezaji wake wamezoeana na kuaminiana kitu kinachofanya timu yake hiyo izidi kuwa bora.

"Nafurahi kuona wachezaji wanaanza kuzoeana na kuaminiana ndio maana timu yangu inafanya vizuri na si kwa mchezaji mmoja mmoja, alisema.

Alisema anawapongeza wachezaji wake kwa juhudi kubwa waliyoifanya katika mchezo huo licha ya kuwa na ushindani ikiwa pamoja na kuushukuru uongozi wake kwa ushirikiano wanaomwonyesha.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >